tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Polepole** atangaza neema soko mafuta ya alizeti Cuba

UKURASA 3




UKURASA 9

Jumapili Septemba 3, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581422
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Vinara wa uhamisho Baraza la Mawaziri

**NI** tangu Samia awe Rais, wako waliobadilishwa wizara mara nne... *Endelea ukurasa. 2*



Dk. Pindi Chana



Dk. Damas Ndumbaro



Innocent Bashungwa



Mohamed Mchengerwa

## Wadaiwa kuvamia zizi, kuchukua ng'ombe kujilipa mahari ya binti



UKURASA 3

## Samia ayapigia debe mashirika ya ndege Afrika kubeba vifurushi

UKURASA 2







Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akikabidhi ufunguo kwa Mtendaji Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU), Sifundo Chief Moyo, kama ishara ya ufunguzi wa jengo jipya la PAPU lenye ghorofa 17, jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

**MICHEZO** KABLA KUWAKABILI AL MERREIKH, GAMONDI ASHTUKIA KITU MAPEMA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Abiria wakiwa kwenye foleni ndefu kusubiri usafiri wa mabasi ya mwendokasi katika kituo cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, Nyakati za asubuhi kumekuwa na foleni kubwa ya abiria kutokana na mabasi hayo, kuwa machache. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vinara wa uhamisho Baraza la Mawaziri

**Na Gwamaka Alipipi**

MAPEMA wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya mabadiliko madogo ya baraza la Mawaziri kwa kuwahamisha baadhi ya mawaziri na naibu mawaziri huku akiwateua wapya na kuwapandisha wengine kutoka nafasi ya naibu mawaziri.

Kubwa zaidi, Rais alianzisha nafasi ya Naibu Waziri Mkuu kwa kumteua aliyekuwa Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, kushika wadhifa huo. Mbali na kuteuliwa katika nafasi hiyo, Dk. Biteko pia ameteuliwa kuwa Waziri wa Nishati.

Sambamba na panguapangua hiyo, kama ilivyo ada, kila yanapotokea mabadiliko ni lazima wawapo watu wanaotemwa kwenye safu ya uongozi na safari hii pia wako waliokumbwa na mabadiliko hayo na kukaa pembeni licha ya kwamba si wengi kama nyakati zingine.

Mawaziri hao ni Mohammed Mchengerwa ambaye amekuwa Waziri wa Nchi TAMISEMI, Balozi Pindi Chana ambaye sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, Innocent Bashungwa (Waziri wa Ujenzi) na Dk. Damas Ndumbaro wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Baada ya kuingia madarakani Rais Samia, Mchengerwa amekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Utamaduni Sanaa na Michezo, Maliasili na Utalii na sasa TAMISEMI. Akizungumza baada ya kuwaapisha mawaziri na makatibu wakuu katika Ikulu Ndogo, Zanzibar, Rais Samia alisema anampeleka TAMISEMI kujiandaa na kivumbi cha uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwakani.

Bashungwa ambaye wakati Rais Samia anaingia madarakani alikuwa Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, ni mmoja wa mawaziri vinara ambao wamekuwa wakiguswa kwenye mabadiliko ya mara kwa mara ya Baraza la Mawaziri.

Mwanasiasa huyo katika uongozi wa Samia, amekuwa pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na sasa Waziri wa Ujenzi.

Waziri mwingine katika orodha hiyo ni Balozi Pindi Chana ambaye katika uongozi wa Rais Samia, amekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii; Utamaduni, Sanaa na Michezo na sasa Katiba na Sheria ambako ndiko taaluma yake.

Dk. Damas Ndumbaro, kama alivyo Balozi Pindi Chana ni mbobezi katika sheria. Naye yuko katika orodha ya mawaziri ambao wameguswa mara nyingi katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri kwenye uongozi wa Rais Samia.

Ndumbaro ambaye alikuwa Waziri wa Maliasili na Utalii wakati Rais Samia anaingia madarakani, aliendelea katika nafasi hiyo kabla ya kupelekwa Wizara ya katiba na Sheria sasa ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aidha, ziko wizara mbili ambazo zimetajwa kuwa zimekuwa zikiguswa kwa kiasi kikubwa kila mabadiliko yanapotokea. Wizara hizo ni Maliasili na Utalii, na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**MALIASILI NA UTALII**

Wizara hii inatajwa kuwa ngumu kutokana na kuwa na nafasi kubwa ya kuguswa pindi kila mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yanapotokea. Licha ya mawaziri wanne katika uongozi wa Samia, mawaziri wengine walioiongoza na miaka kwenye mabano ni Dk. Hamis Kigwangallah (2017-2020), Prof. Jumanne Magembe (2015-2017), Lazaro Nyalandu (2014-2015), Balozi Khamis Kagasheki (2012-2013), Ezekiel Maige (2010-2012) na Shamsa Mwangunga (2008-2010).

Wengine ni Prof Jumanne Maghembe (2007-2008), Anthony Diallo (2005-2006), Zakhia Megji (1997-2005), Juma Ngasongwa (1995-1996), Juma Hamad Omar (1993-1995), Abubakar Mgumia (1990-1993), Marcel Komanya (1989-1990), Arcado Ntagazwa (1987-1989), Getrude Mongela (1985-1987) na Paul Bomani (1984-1985).

Pia wamo Sir George Kahama (1983-1984), Ali Hassan Mwinyi (1982-1983), Isaack Sepetu (1980-1982), Solomon Saibul (1975-1980), Hosnu Makame (1970-1975), Dereck Bryceson (1965-1970) na Tewa S. Tewa (1962-1965).

**TAMISEMI**

Mbali na walioongoza katika awamu ya sita, mawaziri wengine walioongoza wizara hiyo ni aliyeendelea baada ya Samia kuingia madarakani akitokea uongozi wa Magufuli alianza na Waziri Ummy Mwalimu (aliteuliwa na Hayati Rais John Magufuli), ambaye alihudumu kwa kipindi kifupi.

Wengine walioongoza tangu uhuru ni Job Lusinde (1961-1963), Austin Shaba (1964-1965), Oscar Kambona (1965-1966), Peter Kisumo (1966-1971), Paul Kimiti (1984-1985), Kingunge Ngombale Mwiru (1985-1987), Paul Bomani (1987-1989) na Anna Abdallah (1990)

Wengine ni Joseph Warioba (1990-1991), Anna Abdallah (1992-1995), Mussa S. Nkanghaa (1995-1998), Kingunge Ngombale Mwiru (1998-2000), Brigedia Jenerali (Mst) Hassan Ngwilizi (2000-2005), Mizengo Pinda (2006-2008), Steven Wasira (Februari 2008-Mei 2008), Celina Kombani, (2008-2010), Kapteni George Mkuchika (2010-2012), Hawa Ghasia (2012-2015), George Simbachawene (2015-2017) na Selemani Jafo (2017-2021).

# Samia apigia debe mashirika ya ndege Afrika kubeba vifurushi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameuagiza Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kuweka mpango mkakati wa kuyatumia mashirika ya ndege ya ndani ya Afrika kusafirisha vifurushi na barua kuliko kutegemea mashirika ya nje.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa ufunguzi wa jengo la Makao Makuu ya PAPU pamoja na stempu maalum za jengo hilo. Pia aliagiza jengo hilo litumike kufanya uwiano wa maendeleo ya posta za Afrika ili kutoa huduma bora zinazotegemewa na watu wa bara hilo.

"PAPU mnatakiwa kuyafanya mashirika ya posta kuongeza wigo na ufanisi wa usafirishaji kwa kutumia mashirika ya ndege ya ndani badala ya kutumia mashirika ya nje ya Afrika kwa kuwa itatusaidia kuwa na muunganiko ndani ya Afrika.

"Jengo hili litumike kujengeana uwezo na kubadilishana uzoefu, kuongeza ubunifu ili kuleta mageuzi ya kiutendaji posta kwa nchi wanachama kwa kuwa baadhi zimekufa kabisa. Hii sasa itasaidia kuchangia ukuaji mkubwa wa uchumi wa kidijitali na kufanya Umoja wa Afrika kujivunia uwapo wa posta. "Jengo hili la kipekee na lenye hadhi ya juu linafaa kuwa kituo cha maendeleo ya posta za Afrika kuanzia sasa. Natarajia litaleta mabadiliko chanya katika kuandaa mikakati ya namna ya kuimarisha huduma za posta kwa nchi wanachama wa ukanda huu," alisema.

Rais alisema kukamilika kwa jengo hilo, ni matokeo ya ushirikiano kati ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na PAPU na mradi huo ni wa ubia ambapo umoja huo umegharamia kwa asilimia 60 na asilimia 40 zimechangiwa na TCRA.

Pia aliipongeza TCRA na PAPU kwa kutengeneza stempu maalum ya jengo hilo na vivutio vingine na Algeria, Egypt, Morocco, Nigeria, Senegal na Zimbabwe kwa kuchapisha stempu ambazo alizindua kwa kuwa zinaonesha ushirikiano wa dhati kwenye umoja huo.

"Naipongeza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Tanzania pamoja na sekretarieti ya PAPU kwa maandalizi ya mkutano huu wa 41 wa Baraza Kuu la Umoja wa Posta Afrika na wadau mbalimbali walioshiriki na kuchangia kufanikisha mkutano.

"Nimejulishwa kuwa mkutano wenu uliambatana na makongamano mawili yaliyohusu sekta ya posta, wadhibiti, wakuu wa mashirika ya posta Afrika na taasisi nyingine," alisema.

Rais alisema asili ya mawasiliano yote duniani yalianzia katika mfumo wa kiposta ingawa si unaofahamika kipindi hiki kwa kuwa miaka iliyopita mawasiliano kwa njia ya mdomo, ujumbe au maandishi yalibebwa na wanyama wakiwamo punda, farasi na ngamia.

Aliongeza mfumo wa posta wa sasa umeboreshwa kuendana na maendeleo ya binadamu na hadi kufikia karne ya 18, huduma za posta zikawa zimesimamiwa na mifumo ya kitaasisi kwenye ngazi za kitaifa na kimataifa kwa kutumia njia za usafiri wa majini,angani na nchi kavu.

Kwa kutambua umuhimu wa posta kwa maendeleo ya binadamu, alisema mwaka 1874 ulianzishwa Umoja wa Posta Duniani (UPO).

"Baada ya kuasisiwa kwa Umoja wa Nchi Uhuru za Afrika (OAU), viongozi wake waliona umuhimu wa kuanzisha PAPU ili kuzipa msukumo juhudi za maendeleo ya kiuchumi kwa nchi wanachama," alisema.

Alisema wakati maendeleo ya mwanadamu yanavyoendelea kushika kasi, mifumo ya mawasiliano nayo inachukua sura mpya ya kidijitali, hivyo posta haziwezi kubaki kama miaka iliyopita.

Alisema tangu kuanzishwa kwa umoja huo, Tanzania imeendelea kutimiza wajibu wake kwa kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kupitia Sera ya Taifa ya Posta, serikali imejumuisha maendeo ya kijamii na kiuchumi na ukuaji wa teknolojia katika utoaji wa huduma za posta na kubuni huduma mbadala. Pia alisema hatua ya pili iliyochukuliwa na serikali ya Tanzania ni kutekeleza mfumo wa anuani za makazi ambao mwaka 2022 waliendesha zoezi la anuani za makazi kwa nchi nzima.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nauye, alisema serikali ilitoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya umoja huo.

Alisema sekta ya posta imewezesha shughuli za kibiashara, kiuchumi na kijamii miongoni mwa mataifa duniani na kwenye bara la Afrika kupitia majukwaa ya kidigitali huku ikithibitisha jukumu lake na kuwezesha uchumi wa kidigitali.

Waziri Nape alisema umefika wakati wan chi za Afrika kujikomboa kiuchumi kwa kufanya biashara nchi na nchi ndani ya Afrika kwa kuwa kila kitu kinapatikana Afrika.

## HABARI KITAIFA

# Wazazi wadaiwa kuvamia zizi na kupora ng'ombe kujilipa mahari

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

WATU 12 wa familia moja wanadaiwa kuvamia zizi la ng'ombe upande wa ukweni na kuchukua ng'ombe wanne kwa kile kilichodaiwa kujilipa mahari ya binti yao.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:00 alfajiri katika Kitongoji cha Mwamitilwa, Kijiji cha Nyanzumla wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Talime Dioniz, alisema tukio hilo lilitokea nyumbani kwa Charles Joseph ambapo watu hao walifika na kuchukua ng'ombe hao kwa lengo la kujilipa mahari ya binti yao.

Dioniz alisema watu hao walivamia zizi hilo wakiwa wameshika fimbo kwa lengo la kuswaga ng'ombe ambao walitakiwa kutolewa mahari lakini familia ya Joseph ambaye ni mlezi wa kijana anayeoa, Frank Mussa, walikataa.

Taarifa zinasema ndugu hao baada ya kukataliwa, ndipo walianzisha fujo na kuanza kuwatoa ng'ombe katika zizi hilo.

Mlezi wa Frank Mussa (muoaji), Joseph, alisema hajakataa kutoa mahari ya kijana wake lakini wao wamekuwa kinyume cha taratibu na kufanya shughuli hiyo kuwa na vurugu.

"Wamefika usiku tukiwa tumelala wakatusubiri hadi tukaamka na hatukuwa tumepanga siku ya leo (jana) kutoa mahari hiyo lakini nashangaa kwa nini wamekuja kunivamia usiku," alisema.

Charles alisema walielewana kutoa mahari Septemba 15, mwaka huu, ndipo waende kuchukua lakini cha kushangaza walifika nyumbani hapo kabla ya tarehe husika.

Mzazi wa binti anayeolewa, Eli Buluba, alisema alipewa taarifa na kijana ambaye anamuoa binti yake kwamba aende kuchukua mahari ndiyo maana walifika na kuchukua ng'ombe hao.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo aliamua kwenda hadi kwenye zizi hilo na kuanza kuwaswaga ng'ombe kwa lengo la kuchukua mahari.

Mussa alipoulizwa juu ya utoaji wa taarifa hiyo, alikana na kusema hakuwahi kuzungumza na mtu yeyote ukweni lakini alishangaa kuona wakwe zake wamefika nyumbani nyakati za usiku na kuanza kuswaga ng'ombe.

Hata hivyo, watu hao walizuiwa kuchukua mifugo na kesi hiyo kupelekwa kwa wazee ili kushughulikiwa.



Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Tiba Asili cha Saumu Karama, Dk. Saumu Mshewa (kushoto), akitoa maelezo kuhusu tiba kwa watu wenye matatizo ya kuvunjika viungo mbalimbali vya mwili kwa wananchi waliotembelea banda lake, katika maonyesho ya Tiba Asili katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polepole atangaza neema soko la alizeti Cuba

**Na Abeid Makarabo,**
UDSM

BALOZI Wa Tanzania nchini Cuba, Humphrey Polepole amewahakikishia Watanzania kuwapo kwa fursa ya usafirishaji wa mafuta ya alizeti baina ya nchi hizo mbili, kutaleta fedha za kigeni na uwiano wa kiuchumi kwa wafanyabiashara.

Balozi Polepole aliyasema hayo hivi karibuni kwenye mahojiano na kituo kimoja cha televisheni nchini kwamba kuna fursa kubwa kwa wafanyabiashara nchini kuuza mafuta ya alizeti nchini Cuba.

Alisema kutokana na uhitaji huo, wafanyabiashara wa Tanzania wana fursa ya kupeleka mafuta ya alizeti mpaka lita milioni mbili kila mwezi.

"Tunapoagiza mafuta ya kula kutoka nje,tunachukua dola zetu kwenye mzunguko wa ndani na kuzipeleka nje. Tutakapokuwa tunauza nje, tutapata fedha za kigeni na tutapata mlingano mzuri wenye afya kiuchumi," alisema Polepole.

Balozi Polepole alisisitiza kwamba licha ya kuwa Tanzania bado haijajitosheleza katika uzalishaji wa alizeti kwa matumizi ya ndani, fursa iliyopo haitaathiri upatikanaji wa mafuta katika soko la ndani bali itaongeza chachu ya uzalishaji wa alizeti.

"Sisi kama kituo cha uwakilishi Havana tunaamini kwamba mnyororo wa thamani wa bidhaa hii unaanzia kwenye viwanda vikubwa vya kuchakata mafuta, viwanda vya kati na viwanda vidogo vidogo.Tukitafuta soko la mafuta ya alizeti yanayozalishwa nchini tutatengeneza uhitaji wa malighafi, hivyo wakulima wa Tanzania watalazimika kuzalisha alizeti kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya viwanda hivi," alisisitiza.

Balozi huyo pia alitoa wito kwa wadau kuchangamkia fursa hiyo huku akikiri kuwapo ugumu kwenye kupata mpenyo katika soko la dunia jambo ambalo alisema amefanikiwa Cuba na visiwa vya Caribbean.

"Soko la dunia limegawanyika katika maeneo mengi. liko Ulaya, Asia, Marekani na kwingineko. Ugumu katika soko la dunia ni kupata mpenyo wa kuingia. Sisi tumepata soko visiwa vya Carribean, eneo ambalo hatukuwahi kulitegemea kwa haraka kwamba Tanzania ingeweza kupeleka mzigo.

"Sasa hivi tunamalizia utaratibu wa bei pia tunapambana mpaka Novemba, mwaka huu, tuwe tumekusanya makontena 26 mpaka 50 ya mafuta ya alizeti ambayo yatasafirishwa kwenda Cuba kuleta dola nchini.

Mafuta ya alizeti ni bidhaa ambayo itaongeza ukuaji wa diplomasia ya uchumi na biashara kati ya Tanzania na Cuba zikifuatia bidhaa zilizokuwa zikifanya vizuri katika soko kama vile kahawa,korosho, pamba na karafuu.

Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa za COMTRADE, mauzo ya Tanzania kwenda Cuba yalifikia dola za Marekani 30,050 mwaka 2022 huku Tanzania pia ikinufaika na bidhaa zinazoingizwa kutoka Cuba hasa mitambo na mashine mbalimbali zinazotumika katika kilimo, madini na uvuvi.


**NOTICE OF BOARD MEETING**

**THE COMPANIES ACT, 2002 (R.E)**

**(Pursuant to Memorandum and Articles of Association of the Company)**

Notice is hereby given that the meeting of a special meeting of the **PANGANI INDUSTRIES LIMITED** is scheduled on the day of 8th September, 2023 at 10:00 am at Street No. 7/8 Mkwakwani Street Plot No. 40 at Tanga City. The Company invites Directors and shareholders to discuss the issues of dissolution of our Company. Main agenda of the meeting will be to select a liquidator who will supervise the process of Company dissolution.

Bharat Bhagwanji Mulji Laxman (Attorney)
Pangani Industries Limited

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 92 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late: DIONICE KIKOTA LUGAKINGIRA**

**By 1. BERTHA SOSPETER NKAMBWE**
**2.**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 05 day of 09/2023

Dated at MOROGORO this 30 day of 08..2023

RESIDENT MAGISTRATE

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ANNA PETER MALLYA**
anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 187 DGB** aina ya MERCEDES-BENZ yenye CHASSIS NO: **WDB 2030612F209766.** ENGINE NO: **112M26163033.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBD/RB/2563/2023.**

# Ofisa afukuzwa kazi madai kughushi cheti

**Na Rose Jacob,** UKEREWE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe lililojigeuza kamati ya Uamuzi, limemfukuza kazi aliyekuwa Ofisa wa Afya wa Wilaya, Winston Nongwa, kutokana na kughushi cheti cha kidato cha nne kinyume cha sheria na kanuni za nchi.

Sambamba na azimio hilo, baraza hilo limetoa onyo kali kwa Ofisa Utumishi wa Wilaya hiyo, Singo Bakari, na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kamasi, Deus Magesa, kwa kuwakata mshahara wao kwa asilimia 15 kwa kile kinachoelezwa kuwa ni kufanya uzembe katika kazi zao na kuiingizia serikali hasara.

Akisoma maazimio hayo juzi katika Baraza la Madiwani la Robo ya Nne ya Mwaka wa fedha 2023/24, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Joshua Manumbu, alisema baraza limefikia uamuzi huo kutokana na makosa waliyo nayo kila mmoja.

"Ofisa Afya Nongwa anakabiliwa na kosa la kugushi cheti cha kidato cha nne wakati akifahamu kufanya hivyo ni kukiuka matakwa ya sheria, hivyo uamuzi huu ni moja ya majukumu yetu katika halmashauri ikiwa ni pamoja na kusimamia nidhamu na utendaji kazi wa watumishi wote," alisema.

Kwa upande wa Singo, alisema atakatwa mshahara wake kwa asilimia 15 kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kwa kosa la kutokutekeleza maelekezo ya mwajiri wake na kumsabishia hasara ya Sh. 800,000.

Kadhalika, alisema Magesa naye anakabiliwa na adhabu hiyo hiyo kwa kosa la utoro kazini na kwamba adhabu hizo zimetolewa ili iwe fundisho kwa watumishi wa umma.

Aidha, baraza hilo lilitoa onyo kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Selema, Rwegana Matala, kwa wizi wa Sh. milioni 1.5 ambazo ni michango aliyokusanya kutoka kwa wananchi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Selema na ameamriwa kuzirudisha.

Katika hatua nyingine, Baraza hilo lilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na mradi wa BOOST unaoendelea kufanyika katika Kata ya Bukanda kwa kipindi cha robo ya nne 2022/23.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Emmanuel Shelembi, alisema serikali ilielekeza Sh. milioni 100.6 za BOOST kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu matatu ya vyoo. Mradi huo umekamilika kwa asilimia mia moja.

Shelembi alisema pamoja na ujenzi huo, serikali ilipeleka Sh. Milioni 76.6 katika zahanati ya Busunda kwa ajili ya ujenzi wa choo, kichomea taka, mnara wa tangi la maji, upanuzi wa chumba cha kujifungulia wajawazito na sehemu ya kuvalia nguo kwa wanawake wanaojifungua na ujenzi huo uko katika hatua za ukamilishaji.

# Nchi 30 Afrika zanufaika na mtandao wa TTCL

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limesema nchi 30 kati ya 45 wanachama wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU), zimenufaika na kasi ya mtandao unaotolewa na shirika hilo.

Akizungumza juzi jijini Arusha katika maonyesho yaliyoandaliwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yaliyoshirikisha taasisi na mashirika ya umma, Meneja Biashara wa TTCL, Laibu Leonard, alisema moja ya faida za kushiriki maonyesho hayo ni kuendelea kuifungua nchi katika sekta ya utalii.

Alisema nchi hizo zinanufaika na matukio mbalimbali yanayohusu ajenda ya kikao cha 41 cha Baraza la Umoja wa Posta Afrika kinachofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Arusha (AICC).

Leonard ambaye pia ni Meneja wa Banda la Maonyesho hayo, alisema yameandaliwa na wizara hiyo wakati wa kikao cha 41 cha Baraza la Umoja wa Posta Afrika kinachofanyika katika ukumbi wa AICC.Alisema TTCL imeutumia maonyesho hayo kama fursa ya kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwa kuonyesha matukio ya moja kwa moja yanayoendelea huko kuanzia Uhuru Peak.

Leonard alitaja faida ya kushiriki maonyesho hayo kuwa ni kuendelea kuifungua nchi katika sekta ya utalii na kupitia mkutano huo, TTCL imebeba dhamana ya kuhakikisha washiriki wote wanapata mtandao wa uhakika na kasi ikiwa ni dhamira ya shirika shughuli zake kufanyika kidijitali.

"Kupitia mkutano huu wa PAPU, shirika limepata fursa ya kuonyesha huduma zake ukiwamo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) na huduma za Data Center (NIDC). Washiriki wamepata uelewa wa namna miradi hii ya kimkakati inavyothaminiwa na umuhimu wake kwa wananchi," alisema.

Leonard alisema maonesho hayo yanafanyika kuelekea siku ya uzinduzi wa jengo la Makao Makuu ya PAPU uliofanyika jana. Mpaka sasa TTCL imeshafikisha huduma ya faiba katika jengo hilo ili kuhakikisha shughuli zote za kiposta zinatekelezeka kidijitali.

Leonard alisema shirika linatekeleza majukumu yake kuhakikisha miundombinu ya mkongo wa taifa wa mawasiliano inajengwa nchini hadi nje ya mipaka ya Tanzania ili kuziwezesha shughuli za posta ndani na nje ya Afrika kufanyika vizuri.



Ofisa Muuguzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Beatrice Nangawe (kulia), akimpima shinikizo la damu mkazi wa Tabata, Magreth Mwaijala, aliyefika JKCI-Dar Group, kwenye kambi ya huduma ya matibabu bure ya magonjwa ya moyo na yasiyoambukiza, jijini Dar es Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mpango kabambe waja kuokoa watoto njiti

**Na Restuta James**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inakusudia kujenga wodi maalumu za watoto wanaozaliwa na uzito pungufu (njiti) kuanzia vituo vya afya hadi hospitali za rufani, ikiwa ni jitihada za kuboresha huduma za afya nchini.

Aidha, amesema serikali itaendelea kushirikiana na mashirika ya dini na wadau wengine kuboresha huduma za kijamii nchini hususani afya.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa kuhitimisha mbio hizo za Maendeleo Marathon kwa ajili ya kuchangisha fedha za kukarabati Kituo cha Diakonia cha Kilutheri cha Mtoni Mtongani, Dar es Salaam kinacholelea watoto wenye mtindio wa ubongo na usonji.

Fedha hizo pia zimechangishwa kununua vifaa kwa ajili ya wodi ya watoto njiti katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Alisema mipango ya serikali ni kuhakikisha hospitali zote za wilaya zinatoa huduma kwa watoto njiti na kuwasaidia wale wanaozaliwa na usonji pamoja na matatizo mengine, waweze kuongea.

"Tunajenga wodi maalumu kwa ajili ya watoto wachanga pamoja na ununuzi wa vifaa tiba kuanzia vituo vya afya, wilaya, kanda na taifa. Tunahakikisha kila hospitali ya wilaya inatoa huduma za watoto waliozaliwa na uzito pungufu," alisema Majaliwa.

Pia alisema serikali itaendelea kuwaongezea ujuzi wataalamu wa afya walioko kazini na kutoa msaada wa vifaa vya usaidizi kwa watoto wenye mahitaji maalumu.

Alisema serikali inathamini mchango wa sekta binafsi na mashirika ya dini na kuomba ziendelee kushirikiana na serikali katika kuwahudumia wananchi.

Awali, Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya, Prof. Paschal Rugajo, alisema katika kila vizazi hai 100 nchini, 11 ni watoto wanaozaliwa na uzito pungufu na kwamba kwa mwaka, takribani watoto milioni 2.4 huzaliwa na tatizo hilo.

Akizungumzia mbio hizo za hisani, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo, Dk. Ibrahim Mwangalaba, alisema lengo ilikuwa kukusanya Sh. milioni 200 za kukarabati Kituo cha Diakonia cha Mtoni Mtongani na kununua vifaa kwenye wodi ya watoto njiti katika hospitali ya KCMC.

Hata hivyo, alisema zimepatikana Sh. milioni 120 ambazo zimegawanywa sawia katika vituo hivyo viwili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Prof. Gilleard Masenga, alisema hospitali hiyo inalaza watoto 60 hadi 80 kwa mara moja, wenye uzito pungufu na kwamba fedha walizopata zitatumika kuongeza vifaa kwenye wodi hiyo.

Mbio hizo zilizokuwa na kaulimbiu ya 'hatua ya faraja', zilihudhuriwa na zaidi ya watu 3,000 akiwamo Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, Mkuu wa Kanisa hilo Mteule, Askofu Dk. Alex Malasusa, viongozi mbalimbali wa dini, benki na kampuni za bima.

RIPOTI MAALUM – 2

# Anayedaiwa kunajisi mwanawe atoroka akiwa mahabusu polisi

KATIKA toleo letu la jana, kulikuwa na simulizi ya mama, mama wa kambo na daktari aliyemtibu mtoto mwenye umri wa miaka tisa anayedaiwa kunajisiwa na baba yake mzazi wilayani Chamwino, mkoani Dodoma kisha mtuhumiwa huyo kutoroka akiwa katika mahabusu ya polisi. Endelea...

Mtoto amemsimulia mwandishi kwamba, mara ya kwanza kutendwa ukatili huo, baba yake alimwita ndani kisha akafunga mlango kwa komeo la juu, akamlazimisha kuvua nguo huku naye (baba) akivua.

"Aliniambia 'hapa hakuna kutoka nje', akanilalia kifuani... kisha akaniambia 'kesho mama yako akiwa hayupo, nitakufanyia hivihivi'.

"Baadaye akaenda kununua kisu, akanitishia ananichinja. Aliniambia 'ukisema kwa mtu yeyote, ninakuua'. Kwahiyo, nilikuwa ninavumilia.

"Baada ya kuona ninaendelea kupata mateso, nikakimbilia kwa Bamdogo Hamisi, Nilipofika akaniuliza 'kwanini umekimbilia huku?' Nikasema 'baba anataka kunichinja'. Akanipeleka kwa mtendaji, akaniomba namba ya simu ya mama kisha akanipeleka kwa daktari na akampigia mama, akaja kunifuata," anasimulia mtoto huyo.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Juma Mzuri, ana taarifa za tukio hilo. Alishtushwa na taarifa za mtuhumiwa kutoroka katika mahabusu ya polisi na baadaye kufanya utapeli wa Sh. milioni 2.1 kwa mfanyabiashara wa nafaka.

Diwani wa Manzase, John Mika, anasema: "Sijafurahishwa na tukio hilo, kwa sababu ni unyanyasaji, mtu anambaka mtoto wake halafu anapelekwa polisi, muda huo huo anarudi mtaani."

### OFISA MTENDAJI

Akisimulia taarifa za ukatili huo zilivyofikishwa ofisini kwake, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Restuta Kessy, anasema mtoto huyo alifika ofisini kwake baada ya kuelekezwa na ndugu wa baba yake.

Anasema kuwa alipofika alimwambia amechoka kufanyiwa ukatili huo na baba yake na ameshindwa kumweleza mama wa kambo anayeishi naye kwa kuwa baba alimtishia kumuua.

"Alikuja analia, akaniambia 'mimi nimechoka, baba yangu mama akiondoka, ananifanya...' baada ya maelezo hayo, nikampeleka Hospitali ya Mvumi DCT, daktari akathibitisha amebakwa. Nikamkamata mtuhumiwa, nikampeleka polisi kwa ajili ya hatua za kisheria," anasema.



Shekhe Mussa Kundecha.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.

Restuta pia anasema alishtushwa kupata taarifa mtuhumiwa alionekana kijijini kwake siku iliyofuata, na alipohitaji ufafanuzi toka kwa polisi, mrejesho wao - aliwatoroka wakati anakwenda msalani.

Mfanyabiashara wa nafaka anayedaiwa kutapeliwa na mtuhumiwa huyo muda mfupi baada ya kutoroka kituo cha polisi, Winnie Kombe, anadai kuwa wakati anampatia fedha, hakujua kama alikuwa ametoroka mahabusu.

"Mimi ni mfanyabiashara wa nafaka, yule mtuhumiwa ni mkulima hapa kijijini na anafahamika vizuri. Alikuja akaniongopea mtoto wake anaumwa sana, amezidiwa yuko hospitalini mjini.

"Akaniambia 'ninaomba unisaidie Sh. 2,100,000 ili nimnusuru mwanangu, madaktari wanasumbua, utakuja nyumbani kupima mtama, nikamwamini nikampatia'.

"Ikabidi nikimbie niende nyumbani kwake, nikamkuta mke wake, akaniambia 'mbona huyu mtu alikamatwa na polisi? Hayupo hapa'. Nikabaki sina la kufanya kwa sababu mtuhumiwa alipotoroka polisi hakupitia nyumbani, aliingia moja kwa moja mtaani kutafuta wa kumtapeli," anadai.

### WADAU HAKI, SHERIA

Askofu William Mwamalanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashehe ya Maadili Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini, anashauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuanzisha utaratibu mahususi wa kuwatangaza vijijini na mijini wanaume na wanawake wanaopatikana na kesi za kunajisi watoto.

"Kuna kundi la watu wenye 'nasaba ya ubakaji' ambao kila mara hubaka na kushinda kesi. Hii ndiyo siri kubwa ya kushamiri kwa vitendo vya ubakaji kwa watoto. Ni muhimu kuweka utaratibu wa kuwatambua na kuwaweka alama maalum wabakaji ili iwe rahisi kuwatambua," anashauri.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Jumuiya za Kiislamu Tanzania, Shekhe Musa Kundecha, anasema: "Baba anaponajisi mwanawe, anatenda dhambi. Hukumu yake ni kupigwa mawe mpaka kufa. Ndiyo maana maneno ya Mungu yanasema 'usiisogelee zinaa'. Kaa mbali na kila sababu inayoweza kukufanya ukazini.

"Wazazi na walezi lazima wakae vyema na watoto wao, iwe wa kuwazaa au kuwalea, lazima wasitiri faragha baina yao. Zinaa kwa Mwenyezi Mungu ni laana inayomfanya mtu aingie katika moto wa jehanamu.

"Ubakaji ndiyo unaoleta watoto wa mitaani, malezi ya upande mmoja na hayo ni matunda na matokeo ya kutoheshimu maelekezo ya Mwenyezi Mungu," Shekhe Kundecha anaonya.

Anasema kukithiri matendo ya ukatili dhidi ya watoto kunakoshuhudiwa sasa, kumetokana na jamii kutoweka dini kuwa kipaumbele. Dini imekuwa jambo la hiari, na sheria za dini zinaonekana kama siasa kali.

Anashauri serikali iwekeze nguvu katika somo la dini, akiamini watoto wakipewa elimu ya malezi na maadili tangu wakiwa shuleni, vitendo hivyo vitatokomezwa.

Dk. Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ana angalizo lake kisheria, mtuhumiwa kutoroka mikononi mwa polisi ni kosa kisheria. Askari aliyekuwa zamu anapaswa kuchukuliwa hatua za kipolisi.

"Tutakuwa na uhakika gani kama alitoroka? Kama ni kweli katoroka, huyo askari aliyempoteza, anatakiwa achukuliwe hatua na adhabu kubwa. Kama (askari) anaendelea na kazi, inatia shaka kama kweli alitoroka au alimpa chochote kitu amwachie," anasema Dk. Henga.

Mkurugenzi huyo anasema mtuhumiwa akikamatwa, atakuwa na makosa mawili - kunajisi na kumzuia askari polisi kufanya kazi yake, kila kosa lina adhabu yake kisheria.

"Mtuhumiwa huyo amekiuka haki ya malezi, haki za watoto, jinsia, masula ya jinai. Tuhuma zinazomkabili ni kosa kubwa, adhabu yake anaweza kuhukumiwa kifungo cha maisha," anasema.

Dk. Henga anayeeleza kukerwa na ukatili huo dhidi ya mtoto, anashauri wazazi wanapotengana, wafike mahakamani ili chombo hicho kiamue haki ya maelezi, mtoto mwenye umri mdogo aishi mazingira salama.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amoni Mpanju, anabainisha kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto ikiwamo kuwanajisi.

Anarejea takwimu za Jeshi la Polisi kwamba kwa mwaka 2022, kulikuwa na makosa 12,163 ya kimaadili yaliyotendeka dhidi ya watoto. Kati yake, ya ubakaji ni 6,335, ulawiti 1,575 na ndoa za utotoni 1,555.

"Hii si ishara njema, tunaitaka jamii kutoa ushirikiano. Tunawekeza nguvu zaidi katika kuzuia na huwa tunachukua hatua za kisheria kwa waliofanya vitendo hivyo.

"Tumewekeza katika kutoa elimu, ikiwamo shuleni, vyombo vya habari, semina na mikutano ya kisiasa. Viongozi wa dini watusaidie kupitia nafasi kusema na wazazi watimize wajibu wao," anasema.

Wakili Mpanju anahimiza wazazi kutimiza wajibu wao wa malezi bora kwa mtoto katika kumjali, kumlinda, mawasiliano na ushirikishwaji wa mtoto.

"Tujifunze kudhibiti tamaa zetu, haiwezekani nchi hii ina wanawake wengi halafu mtu anakwenda kumbaka mtoto wake," anaonya.

Ukatili uliotendwa dhidi ya mtoto huyo unakinzana na sera na sheria za nchi. Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 inaelekeza ni kinyume cha sheria kufanya vitendo vya ubaguzi, unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto.

Sheria inaelekeza mtoto alindwe, kwa matunzo na haki, kulelewa na wazazi, kupewa jina kuwa na utaifa, kupata mahitaji ya msingi kama chakula, malazi, mavazi, matibabu, chanjo, elimu na haki ya kucheza na kuburudika.

Vilevile, Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2008 inaelekeza mtoto apewe haki ya kuishi, kudekezwa, kulindwa, kushirikishwa na kutobaguliwa.

Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, kifungu cha 131(3), inaelekeza adhabu kwamba "mtu yeyote atakayetenda kosa la kubaka msichana wa chini ya umri wa miaka kumi (10) atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha gerezani."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la nyumba za askari polisi lichukuliwe kwa uzito

**JESHI** la Polisi nchini ni chombo muhimu katika kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unadumishwa na kuimarishwa. Kutokana na hali hiyo, ili jeshi hilo lifanye kazi zake kwa ufanisi ni lazima liwezeshwe kwa kuwa na vitendea kazi bora na askari wake wanakuwa na maslahi mazuri.

Kama mambo hayo hayatafanyika kwa ufanisi ni dhahiri kwamba ile dhima ya jeshi hilo katika kulinda raia na mali zao pamoja na kupambana na uhalifu, itakuwa ndoto za mchana.

Hata hivyo serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha askari polisi, kuanzia wa chini mpaka ngazi za juu, wanawezeshwa kwa kupatiwa vifaa kama vile magari pamoja na maslahi bora. Licha ya juhudi hizo, baadhi ya askari wameharibu sifa nzuri za jeshi hilo kwa kutuhumiwa kushiriki vitendo viovu kama vile kubambikia raia kesi, kujihusisha na ujambazi, kuomba na kupokea rushwa. Mambo hayo hayaondoi wajibu wa polisi kufanya kazi ndiyo maana bado wanaendelea kutimiza majukumu yao.

Pamoja na hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa kuhakikisha utendaji unakuwa wa viwango, juzi liliulizwa swali bungeni kuhusu mpango wa serikali kujenga nyumba za askari polisi kutokana na kuwapo kwa tatizo eneo hilo. Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, aliuliza swali hilo kwamba kuna tatizo la makazi ya askari polisi katika jimbo lake akitolea mfano wa kata kadhaa kwenye wilaya ya Ikungi.

Katika swali lake hilo, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za askari polisi hususan wilaya ya Ikungi kutokana na wengi wao kupanga nyumba uraiani. Hakuishia kwa askari wa chini pekee bali alikwenda mbali zaidi kwa kusema hata mkuu wa polisi wa wilaya (OCD) naye anakaa katika nyumba ya kupanga.

Katika wilaya hiyo hakuna nyumba hata moja ya askari na hata Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya analazimika kupanga nyumba mtaani.

Pia, alihoji lini Serikali itajenga vituo vya Polisi kwenye kata za Mkiwa, Misughaa na Mungaa kwenye jimbo hilo kutokana na ukuaji wa kiuchumi unaoongeza matatizo ya kiusalama kwenye maeneo mbalimbali.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, akijibu swali hilo kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, alisema mkakati wa serikali ni kuhakikisha askari wanaishi maeneo stahiki karibu na maeneo ya kazi na kwamba katika kutekeleza hilo, serikali katika bajeti zake, itaendelea kutenga fedha kwa ajili hiyo. Alisisitiza kuwa serikali ina taarifa za kukosekana kwa nyumba za makazi ya polisi na kwamba maeneo yametengwa sehemu mbalimbali ili kujenga nyumba hizo.


Suala la makazi ya polisi ni nyeti kutokana na ukweli kwamba askari hao wanapaswa kuwa na makazi bora ambayo yatawawezesha kuishi bila bughudha na kuwa katika hali ya usalama. Kukaa uraiani tena nyumba za kupanga, ni kuhatarisha usalama wao kutokana na ukweli kuwa moja ya kazi kubwa wanayofanya ni kupambana na uhalifu, hivyo kukaa uraiani kunahatarisha maisha yao.

Ni vyema serikali ikalichukulia suala hili la makazi ya askari polisi kwa uzito mkubwa ili kuwaweka katika mazingira mazuri ya kufanya kazi. Mkazo mkubwa katika hili, uelekezwe zaidi katika wilaya mpya zilizoanzishwa miaka ya karibuni ambazo hazina nyumba za kutosha za askari polisi.

Katika kufanikisha suala hili, unaweza kuandaliwa mpango shirikishi baina ya serikali na wananchi pamoja na wadau wengine wa maendeleo. Ni imani kwamba iwapo jambo hili litawekewa mikakati sahihi, linaweza kumalizika ndani ya muda mfupi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Kausha damu' ni kikwazo maendeleo ya wanawake



Na Sabato Kasika

**KWA** muda mrefu wanawake wamekuwa wakilalamikia mikopo ambayo huchukua kutoka vikundi binafsi vinavyokopesha fedha, kwamba inasababisha ugumu wa maisha kutokana na masharti yake.

Mikopo hiyo inaelezwa pia kwamba inachangia baadhi ya wakopaji kupoteza hata vitu katika nyumba zao, wengine kufikishwa mahakamani kwa kuchelewa kurejesha fedha za mikopo hiyo yenye riba kubwa.

Kupitia mikopo hiyo, mkopaji awe hajafanya biashara kwa sababu ya kuumwa au vinginevyo, ni lazima arejeshe fedha kila siku, na kwamba kama hana rejesho, ni lazima akimbie kutoka kwake kwenda kujificha.

Asipokimbia wakopeshaji na wanachama wenzake katika kikundi watamfuata ili atoe marejesho na kama hana, lazima atakimbia kuepuka kuchukuliwa vitu vyake kama dhamana ya mkopo.

Kwa ujumla, hiyo imekuwa sehemu ya maisha ya wakazi hasa wa Dar es Salaam, ambao wanategemea mikopo aina hiyo kwa ajili ya kuendeshea biashara zao.

Wakati wakiwa katika mazingira hayo, juhudi mbalimbali zimeanza kufanyika ili kuwatoa huko, ikiwamo kuwaelimisha ili waende katika taasisi za fedha zenye mikopo yenye masharti nafuu na riba kidogo.

Shirika lisilo la kiserikali la Himiza Development Organization (HDO), ni miongoni mwa wadau wanaotoa elimu kwa wanawake kwa kushirikiana na Benki ya Azania ili waweze kufungua akaunti iitwayo 'Mwanamke Hodari', kuwawezesha kupata mikopo ya riba nafuu.

Ninadhani hiyo ni fursa kwa wanawake kuchambua mbivu na mbichi kati ya mikopo wanayolalamikia kuwa inawaumiza na ile ya benki kuona ni wapi penye unafuu ili waamue cha kufanya.

Lengo ni kupata unafuu, hivyo iwapo watabaini kuwa hata huko kwenye benki kuna ugumu, basi watafute njia nyingine yenye unafuu ili maisha yaendelee, kuliko kuumizwa na hiyo mikopo ya mitaani.

Ikumbukwe kuwa serikali ilisitisha utoaji wa mikopo wa asilimia 10 wa halmashauri kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu baada ya kubaini uwapo wa kasoro mbalimbali katika utoaji.

Kwa hatua hiyo, ni wazi kuna vikwazo vingi ambavyo wakopaji wanapitia ambavyo vinawafanya wasipige hatua kimaendeleo na kujikuta wakiwa kama wanawanufaisha wakopeshaji.

Hivyo, ninadhani kuna haja ya kuendelea kuwasaidia kupata taasisi nyingi zaidi za kifedha zenye akaunti rafiki kwao, ili wasahau machungu ambayo wamekutana nayo kupitia kausha damu au kaza roho na kusababisha waendelee kuumia.

Lakini pia, sidhani kama Azania peke yake inaweza kujitosheleza kuwahudumia wanawake wote nchi nzima wanaohitaji mikopo, bali njia nzuri kila taasisi ya fedha kuibuka na mbinu ya kuwawezesha.

Vilevile, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima alishawataka wanawake wanaolia kuhusiana na mikopo hiyo kutafuta fursa nyingine kupitia majukwaa ya uwezeshaji kiuchumi wanawake.

Lengo ni kuhakikisha wale wote wanaolia mikopo isiyoeleweka, wanapata fursa nyingine za mikopo nafuu kupitia majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi yanayojulikana zikiwamo benki.

Inaelezwa kuwa mikopo ya 'kausha damu, roho mikononi' na mingine ya aina hiyo, ni rahisi kupatikana, kwa kuwa mtu anaweza kwenda kukopa na kuipata siku hiyo hiyo bila usumbufu.

Lakini ukweli ni kwamba, inaumiza na inadhalilisha kutokana na riba yake, masharti pamoja na nguvu inayotumiwa na wakopeshaji kudai marejesho pale mteja anapochelewa kurudisha rejesho kwa wakati.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Nini maana ya Katiba ni sheria mama?



Pascal Mayalla

SEHEMU ya kwanza wiki iliyopita, ilitambulisha nini maana ya Katiba, ni ya nani na ya kazi gani. Katiba ni mkataba wa watawala na watawaliwa ni ya wananchi na kazi yake ni kutoa maelekezo ya kila kitu kitakavyofanyika. Kwa mantiki hiyo, Katiba iko juu ya kila kitu. Hakuna aliye juu ya katiba. Pia nilionyesha viongozi wetu na mihimili yake ilivyojiinua juu ya Katiba na hata kukiuka Katiba yenyewe.

Leo katika sehemu ya pili najadili dhana ya Katiba ndiyo sheria mama. Ibara ya 64(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya mwaka 1977, inasema Katiba ndiyo sheria mama. Sheria nyingine yoyote inayokwenda kinyume cha Katiba ni batili na ikitokea sheria nyingine yoyote ikakinzana na Katiba, basi Katiba ndio itasimama. Kwa Kiingereza dhana hii inaitwa 'The supremacy of the constitution', yaani hakuna aliye juu ya Katiba, msimamo wa Katiba ndio juu ya kila kitu.

Mfumo wa uongozi wa Tanzania ni kupitia mfumo wa mihimili mitatu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii yote mitatu kinadharia iko sawa na inalingana. Kila mhimili una wajibu wake, nguvu zake na mamlaka yake inayojitegemea, kwa kufanya kazi bila kuingiliana, Bunge kazi yake ni kutunga sheria na kuisimamia serikali, Mahakama kazi yake ni kutafsiri sheria na kutoa haki, Serikali kazi yake ni kutekeleza sheria na kuzihudumia Bunge na Mahakama.

Rais ni mkuu wa mhimili wa Serikali, Spika ni mkuu wa mhimili wa Bunge na Jaji Mkuu ni mkuu wa mhimili wa Mahakama. Wote wanakula kiapo cha kuongoza kwa mujibu wa Katiba ya JMT na kuapa kuilinda na kuitetea na kumwomba Mungu awasaidie.

Waanzilishi wa mfumo huu pia waliuwekea mfumo wa ukiranja, yaani 'checks and balance' kwa kila mhimili kuwa kiranja wa mhimili mwingine ili usikiuke mamlaka yake au kuvuka mipaka. Kanuni hii kwa Kiingereza inaitwa 'The doctrine of separation of powers, check and balances'.

Kwa hiyo Katiba ndiyo kila kitu na kwa vile Katiba ni mali ya wananchi, ina maana wananchi ndiyo kila kitu. Viongozi ni watumishi wa wananchi lakini kutokana na madaraka na mamlaka ya viongozi wetu, baadhi yao wamejiinua na kujiona ndiyo kila kitu na wengine kufikia hata kuikanyaga Katiba.

Dhana ya Katiba ni sheria mama na sheria nyingine yoyote inayokwenda kinyume cha Katiba ni batili, dhana hii kwa jicho la mtunga Katiba, alimaanisha kwamba ikitokea ikatungwa sheria yoyote inayokwenda kinyume cha Katiba, sheria hiyo inakuwa batili mara moja. Anayebatilisha sheria hiyo si Mahakama, Bunge wala Serikali bali ni Katiba yenyewe kupitia ibara hiyo ya 64 (5).

Kwenye sheria batili inayokwenda kinyume cha Katiba, jukumu la Mahakama ni kutafsiri Katiba na kutangaza sheria fulani ni batili. Baada ya Mahakama kutangaza ubatili wa sheria fulani, baada ya tangazo hilo, sheria hiyo inakuwa umebatiliswa na Katiba na si Mahakama.

Si mara moja wala mbili, serikali yetu imekuwa ikipeleka Bungeni miswada ya sharia. Baadhi ya miswada hiyo ina vipengele batili vinavyokwenda kinyume cha Katiba yetu. Swali la kujiuliza inawezekana vipi serikali yetu yenye wanasheria mabingwa wabobezi na wabobevu kutunga muswada wa sheria batili inayokwenda kinyume cha Katiba?. Jibu ni kwamba watunga miswada ya sheria, hawajui vizuri na kikamilifu Katiba ya JMT.

Baada ya serikali kutunga miswada ya sheria batili, Bunge letu tukufu ambalo nalo limeshehenezwa na wanasheria manguli wabobezi na wabobevu, nao pia wanaitunga hiyo sheria batili na kumpelekea Rais kutia saini na kuwa sheria!. Swali ni je, inawezekana vipi Bunge letu Tukufu lenye wanasheria mabingwa wabobezi na wabobevu kutunga sheria batili inayokwenda kinyume cha Katiba?. Jibu ni moja tu kwamba watunga sheria wetu nao pia hawajui Katiba ya JMT kikamilifu.

Mtu pekee ambaye hana kosa katika hili la sheria batili ni Rais wa JMT kwa kutia saini sheria batili inayokwenda kinyume cha Katiba kuwa sharia kwa sababu naye ana wasaidizi anaowaamini, hivyo sheria batili hizo zikifika mezani kwake, anaanguka tu saini na zinakuwa sheria.

Kama watu waliopaswa kuijua Katiba hawaijui, watu wanakula kiapo cha kuilinda na kujitetea katiba ya JMT ndio hao wanaikanyanga, unategemea nini kwa mwananchi wa kawaida kuijua Katiba?. Kwa hiyo elimu hii ya Katiba ya JMT ni muhimu sana kwa wananchi ili kuijua.

Baada ya Bunge kutunga sheria batili, kuna mwananchi mzalendo wa kweli wa taifa hili, alifungua shauri Mahakama Kuu kupinga sheria batili hiyo, akashinda. Mahakama Kuu ilitangaza ni batili na kutoa amri ifutwe kwenye vitabu vya sheria. Mzalendo yule hakukubali katiba yetu inajisiwe, akafungua shauri lingine kupinga mabadiliko hayo, Mahakama Kuu ikampa ushindi, ikatangaza mabadiliko hayo ya katiba ya JMT ni batili.

Serikali haikukubali ikakata rufani katika Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi huo wa Mahakama Kuu, kutamka kipengele cha Katiba ni batili. Mahakama Rufani

ikawaita manguli watatu wa sheria kuwa marafiki wa Mahakama, ambao kisheria huitwa "Amicus Curiae" ikatoa uamuzi wa ajabu uamuzi kuwahi kutokea kwenye historia ya mahakama zetu, ambao nauita ni uamuzi sarakasi.

Mwanzo nilisema mihimili hii mitatu ina wajibu wa kuheshimiana na kutoingiliana lakini kila mhimili ni kiranja wa mwingine kupitia kanuni ya 'the doctrine of Separation of powers, checks and balances'. Serikali ikikiuka mamlaka yake inadhibitiwa na Bunge na Mahakama. Bunge lilikiuka mamlaka yake inadhibitiwa na Serikali na Mahakama, Mahakama nayo ikikiuka mamlaka yake, inadhibitiwa na Bunge na Serikali.

**Je, sheria hiyo batili ni ipi na ubatili wake ni upi na una madhara gani? Tukutane wiki ijayo.**

**Paskali**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Chifu Hangaya kwa Biteko ameupiga mwingi



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KUNA kamchezo fulani nakasikia kanatokea wizarani, kuna wakurugenzi wenye magari ambao stahiki yenu ni kuwa na gari kama ambavyo RMO (Mganga Mkuu wa Mkoa) una hadhi ya kuwa na gari.

"Inatokea Mkurugenzi hana ratiba ila wafanyakazi wake wa chini wanakwenda safari, haruhusu gari litoke kwa sababu anadhani bila yeye kuwamo, matairi hayazunguki. Huo ni ushamba!

"Hizi mali ni za serikali. Siku ukijua kutofautisha mali za serikali na wewe havitakuumiza kichwa. Kama kuna ofisa wako anatakiwa kwenda kazini nje ya ofisi, kuna gari lako, Prado jipya, V8 lako na wewe huna ratiba nyingine, una shida gani uko Dodoma pale ukapanda gari la kawaida, halafu vijana wanakwenda wakafanye kazi tukaongeza tija?

"Ile hali ya kuamini, kwamba ni gari langu ni ushamba, hili ni gari la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa wakati huo wewe umewekwa humo, kwa maana gani, inawezekana baada ya nusu saa usiwe wewe, akawamo mwingine.

Kwani unapungukiwa nini siku moja nawe ukapanda gari la wafanyakazi ukiwa Mkurugenzi, utaishiwa oksijeni?

"Lakini kuna watu bila lile gari... kwanza anataka akichungulia alione limeegeshwa pale. Na anataka kutoka anampigia dereva aliwashe, alikute linanguruma.

Ni ushamba tu! Hili gari ni la serikali, litumie ukijua ni mali ya umma.

"Wapo wakurugenzi wengine, hata hela ya mafuta anayo yeye, amekaa kwenye kiti anachungulia geji, anataka kibaki kitu. Nao ni ushamba! Mpe dereva ashike, mpe dereva ashike hela ya mafuta na ya service, kazi yako ni kufikishwa unakokwenda."

Hii si kauli ya mwingine, bali ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Daktari Dotto Biteko, aliyoitoa akiwa bado Waziri wa Madini wakati akizundua magari mapya ya serikali mahali fulani hivi ambako waliokuwapo watakumbuka.

Ni kauli nzito ya kiuongozi lakini pia yenye mamlaka si ya ubabaishaji. Kwa kuitafakari, utaona kuwa huyu ni kiongozi anayefikiria na asiye mjivuni katika utekelezaji wa majukumu yake.

Hakika ni kiongozi asiyeendekeza anasa na ambaye haoni soni kukaa na wananchi wa kawaida na kufanya nao kazi, na ndiyo sababu anawashangaa wakurugenzi wa aina hiyo ambao hutaka kuhodhi mali za Serikali, kana kwamba ni zao, wakijisahaulisha kuwa cheo ni dhamana.

Sitaki kuamini kwamba Daktari Biteko alikuwa anaigiza au anafurahisha kikao bali alikuwa akimaanisha baada ya kuona tabia za wengi wa viongozi wetu zilivyo na si tu kwa ngazi ya ukurugenzi lakini hata katika ngazi za juu za uongozi, wakiwamo baadhi ya mawaziri.

Tunawaona viongozi ambao zamani tukiwa nao mitaani walishuka mabega, lakini baada ya kupewa dhamana wakayapandisha na kudharau wanaowaongoza, wakiwamo hata waliowapigia kura na kuwachagua katika nafasi walizonazo.

Nasema, Daktari Biteko huyu pamoja na nafasi aliyopewa hivi karibuni na Chifu Hangaya, hatabadilika na ndipo sasa atakuwa karibu na wananchi na kusikiliza na kutatua kero zao akimsaidia bosi wake, Kassimu Majaliwa.

Si wengi walioamini kwamba katika kipindi hiki, Chifu Hangaya angeweza kufanya mabadiliko kama alivyofanya na hasa kumpa Daktari Biteko nafasi hiyo kwa sababu tumezoea kuona wenye makeke ndio wakiteuliwa na kuachwa watulivu na wakimya kama huyu.

Tunasahau kuwa kimya kingi kina mshindo, hivyo ndivyo alivyoona Rais Samia Suluhu Hassan na kumpa cheo hicho kijana huyu, ambaye msimamo wake unaakisi kabisa misimamo ya watu watokao ukanda atokao yeye.

Tulizoea sana kuona baadhi ya viongozi wenye uswahiliswahili, waongowaongo wanaosema leo hili na kesho lile, wakijali zaidi matumbo yao na si shida za wananchi, na matokeo yake ni kuichukia Serikali waliyoiingiza madarakani wenyewe.

Nadhani Daktari Biteko anajua njia anayoifuata na atawaelekeza wengine kufuata, ili kuona wananchi wanatendewa wanachokitarajia na kukitaka, ikiwa ni pamoja na kuletewa maendeleo ambayo ndiyo matamanio yao makubwa katika maisha yao.

Kwa kuwa na unyoofu katika msimamo, basi Chifu Hangaya ajue hajapoteza kwa kumtwisha jukumu hilo zito kama ambavyo hata Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini Tanzania (STAMICO), Daktari, Venance Mwasse alivyotwambia hivi karibuni, kuwa bila Daktari Biteko shirika lake lisingechomoka shimoni lilimokuwa.

Daktari Biteko apewe tu ushirikiano katika majukumu yake mapya, huku tukiamini kwamba kama alivyofanya akiwa Madini atafanya vivyo hivyo Nishati, ili tusikose mafuta jamii ya petroli na umeme ukome kukatikatika kama ilivyokuwa.

**Alamsiki!**

# Kinamama Kimasai wapatiwa fedha vyerehani kujikwamua kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

VIKUNDI 11 vya wanawake jamii ya Kimasai katika Kata ya Kimokouwa, Longido mkoani Arusha vimepatiwa Sh. milioni 22 ili kuendeleza na kukuza mitaji ya biashara zao za ufugaji, kilimo na vikundi vya akiba na mikopo (VICOBA).

Kadhalika, vikundi hivyo vimepokea cherehani 11 zitakazotumika kutengenezea taulo za kike kwa ajili ya wasichana 1,412 katika shule za sekondari za Namanga na Lekule.

Fedha na cherehani hizo zimetolewa na Shirika la Legal Services Facility (LSF) kwa kushirikiana na Taasisi ya North-South Cooperation kutoka Luxembourg.

Akizungumza wakati wa hafla iliyofanyika juzi Longido, Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema msaada huo umetolewa kupitia mradi wa miaka miwili wa mwaka 2023/24 unaotambulika kama 'Wanawake Tunaweza' ambao ulizinduliwa Januari, mwaka huu.

Ngw'anakilala alisema mradi huo unatekelezwa wilayani Longido kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake na jamii ya Kimasai nchini katika nyanja ya kiuchumi na kijamii.

"Mradi huu umelenga kufanya kazi na wanawake kupitia vikundi vya wanawake kwa kuwajengea uwezo katika masuala ya kibiashara na ujasiriamali pamoja na kuwawezesha kupata soko la bidhaa mbalimbali watakazozizalisha," alisema na kuongeza kuwa mradi huo unawawezesha watoto wa kike kupata elimu bora kwa kuwezesha ujenzi wa majengo.

Alisema LSF imewawezesha wanawake wanane ambao ni wawakilishi wa vikundi vya wanawake katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi cha Mariale kwa ajili ya kupata ujuzi wa ushonaji nguo, mafunzo hayo yatafanyika kwa muda wa mwezi mmoja.

Pia alisema LSF imezindua ujenzi wa mabweni mawili ya wasichana, moja katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lekule utakaogharimu Sh. milioni 140 na lingine katika Shule ya Sekondari Namanga kwa gharama ya Sh. Milioni 120.

Ng'wanakilala alisema shirika hilo limeamua kutekeleza mradi huo kwa kushirikiana na wadau wengine ili kusaidia jamii ya kimasai hususani wanawake na watoto wa kike, ambao wamekuwa nyuma katika hatua za maamuzi, umiliki wa rasilimali ikiwamo ardhi na mifugo, pamoja na fursa sawa ya kwenda shule.

"Jamii ya kimasai ni ya kipekee nchini Tanzania kutokana na udumishaji wa mila na desturi zake kwa kipindi kirefu. Uchumi wa jamii ya kimasai unategemea zaidi shughuli za ufugaji kwa asilimia 85 ya shughuli zote za kiuchumi zinazoendeshwa na jamii hii.

"Njia kuu za uchumi pamoja na uzalishaji mali kwa jamii ya kimasai zinamilikiwa na kuendeshwa na wanaume, hali inayosababisha haki za wanawake na wasichana wa kimasai kukiukwa," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Dominic Ruhamvya, aliwapongeza wadau hao kwa kuona vyema na kuamua kushirikiana kutekeleza mradi huo na kueleza kuwa, ujenzi wa mabweni utawezesha kutatua changamoto ya watoto kubanana na kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu utakaochochea ufaulu kuongezeka.

Pia alisema hatua hiyo itaviongezea nguvu vikundi hivyo kujikita katika shughuli za uzalishaji na kuwainua kiuchumi, kutoa huduma bora na malezi kwa watoto na hatimaye kukuza ustawi wa jamii nzima kwa ujumla.




Mbunge mstaafu wa Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Hebert Mntangi akizungumza na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uzinduzi wa harambee ya ujenzi wa ofisi ya chama ya kata ya Misozwe jana. Kushoto ni Diwani wa kata hiyo, Jestina Mntangi na (kulia) ni Mwenyekiti wa CCM kata hiyo, Paul Jeremia. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mtoto adaiwa kuunguzwa makalio na mjomba

**Na Beatrice Shayo**

MTOTO mwenye umri wa miaka mitatu, anadaiwa kufanyiwa ukatili na mjomba wake kwa kumuunguza na maji ya moto katika makalio na kumfanyia kipigo katika kijiji cha Msowero, Kilosa mkoani Morogoro.

Mtoto huyo kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Mtakatifu Joseph, Dumila tangu Agosti 27, mwaka huu, huku ikidaiwa kuwa mjomba anayedaiwa kufanya kitendo hicho amekimbia.

Caroline Makemo, aliyejitolea kumlea mtoto huyo baada ya kufanyiwa ukatili huo, ambaye ni mkazi wa kijiji cha Dumila, alisema jana kuwa mtoto huyo amemtoa kijiji cha Msowero akiwa amefanyiwa kitendo hicho.

Alisema alipigiwa simu na Mtendaji wa Kata ya Msowero kwa ajili ya kumchukua mtoto huyo Agosti 27, mwaka huu, na kumjulisha kuwa amechomwa na moto kwenye makalio na miguu na mlezi wake huyo.

Makemo alisema alijulishwa hali ya mtoto si nzuri kwa sababu bado hajapatiwa matibabu na kumwomba aende kumchukua.

"Kwa vile mimi ni mlezi wa watoto nina kituo cha watoto yatima, nilikwenda kumchukua mtoto huyo kwa barua niliyopewa na ofisa mtendaji. Ilinibidi nimuulize mtendaji mtoto huyo imekuwaje ikabidi tumtafute mjomba ambaye ni mlezi wake nikajulishwa kuwa amekimbia.

"Nikauliza shangazi yuko wapi nikajulishwa yupo nikamwona na nikafanya naye mahojiano. Nilimuuliza mtoto amefanyaje akaniambia ameungua akiwa ameondoka kwenda kuchuma mboga na alivyorudi alimkuta amelowa na kwamba aligundua baada ya saa tatu kupita," alisema.

Makemo alisema shangazi huyo alidai aliuliza kwa watoto wenzake mbona amelowa akajulishwa ameungua akachukua jukumu la kumvua nguo na kumpaka tope kama huduma ya kwanza.

"Nilimwambia shangazi unanidanganya. Haiwezekani mtoto aungue na moto kwa madonda haya ukae masaa matatu usijue ukiwa kama mlezi. Yule shangazi akaniambia aliipua viazi na kuweka chini na watoto walikuwa wanakunywa chai, hivyo wakati wanarudisha vikombe akaangukia viazi alivyokuwa ameweka chini," alisema.

Makemo alisema alimjulisha maelezo aliyompatia hayajamridhisha kwa sababu ya ukubwa wa kidonda alicho nacho mtoto asijue maumivu yake yametokana na nini.

Alisema kwa kuwa lengo lake ni kumsaidia mtoto huyo, alimchukua na kumpeleka katika hospitali hiyo kwa kuwa kidonda kilikuwa kinatoa harufu, usaha na kuwapo uvimbe makalioni.

Hali hiyo, alisema ilimpa picha kuwa mtoto huyo hakupelekwa hospitalini na alipouliza alimjulisha hajapelekwa na aliishia katika duka la dawa. Pia alisema kwa sasa mtoto huyo amefanyiwa matibabu na dalili ni nzuri hata harufu aliyokuwa nayo haipo na maumivu yamepungua.

"Huyu mtoto alikuwa na maumivu makali hata usiku sikulala tulivyokuwa hapa hospitalini. Kwa sasa hali inaenda vizuri hata ile harufu aliyokuwa nayo haipo," alisema Makemo.

Makemo alisema aliuliza mama wa mtoto akajulishwa amepatwa na tatizo la akili na baba yake hajulikani aliko. Alisema hadi sasa bado hajawapata ndugu wa mtoto huyo na mjomba wake aliyekuwa anamlea amekimbia amejiuliza kwa nini akimbie.

Makemo ameiomba serikali iwasaidie wale ambao wanaibua matukio hayo ili mtuhumiwa akamatwe na kuchukuliwa hatua iwe fundisho na kwa wengine.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Yunfa Hezron, alisema wamempatia mtoto matibabu na kwa sasa hali yake inaendelea vizuri ikilinganishwa na awali.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka, alisema analaani vikali kitendo hicho cha kusikitisha kinachoonyesha mtoto huyo amepitia madhila makubwa.

"Wakati tunamjulia hali na kumuangalia kilichomsibu inaonyesha amemwagiwa maji ya moto katika maeneo yake ya makalio na kuathiriwa baadhi ya maeneo yake ya mwili. Nimezungumza na mtoto anaeleza bahati nzuri mtoto ukimfanyia ubaya anajua amenieleza aliyemfanyia hilo tukio ni mjomba wake," alisema.

Shaka alisema serikali itasimamia matibabu ya mtoto huyo kama inahitajika kupelekwa hospitali kubwa zaidi ili arudi katika afya yake. Alisema hata baada ya matibabu serikali itaendelea kumwangalia kuhakikisha anapata haki zake za msingi.

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana

JUMAPILI SEPTEMBA 3, 2023


Nipashe *Jumapili*




# MAJIRA YA JOTO HAYOO




## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | |
|---|---|
| TIMBA | SIMBA |
| LUKU | KUKU |
| TUNDA | PUNDA |
| KATA | BATA |
| PIMA | KIMA |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| N | ■ | P | I | C | H | A |
| I | ■ | ■ | ■ | H | ■ | H |
| P | ■ | A | R | A | ■ | S |
| A | L | E | ■ | P | U | A |
| S | ■ | N | O | A | ■ | N |
| H | ■ | D | ■ | ■ | ■ | T |
| E | L | E | W | A | ■ | E |


## AMSHA AKILI



| | |
|---|---|
| KITABU | |
| GOLI | |
| FUNGUO | |
| BARUA | |




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

TAA, FAA, SAA, MTI, IBANE, JIONI, FATWA, OBAMA, ALASIRI, IMBISHA

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kulima bustani ya mboga pembeni ya nyumba yao. Wakati wanalima Juma alianza kumuuliza mama yake.

Juma: Eti mama ni kweli mchuma janga hula na wakwao?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima watakula pamoja

Juma: Kwani janga ni tunda hadi ale na ndugu zake?

Mama: Mwanangu huo ni msemo unaomaanisha kila baya unalolitafuta, utaathirika pamoja na ndugu zako, hivyo ni lazima kujiepusha.

**SWALI**

Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Wanawake wanavyotumiwa na shetani kuvuruga wenzao

KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya pili kuhusu mbinu ambazo shetani huzitumia kumshambulia wanawake. Wiki iliyopita nilitaja mbinu kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwatupia roho za kichawi.

Utafiti unaonyesha kuwa uchawi upo sana kwa wanawake. Kutokana na roho hiyo ya uchawi, wengi wanaishi maisha mabaya sana. Nikataja mchawi asiyejifahamu, aliyelazimishwa, majini mahaba, upweke, roho ya kuachika.

Mbinu nyingine nilitaja roho ya ukoo na familia, matatizo ya uzazi, roho ya kukataliwa, maagano ya kuzimu na afya mbaya. Leo niongezee mbinu zingine anazotumia shetani kumpiga mwanamke.

Ziko laana zinazotesa wanawake. Ni muhimu kutambua kuwa pale tu mwanamke anapoanza kupambana na nguvu zilizokusudia kumwangusha na kuua hatma yake, atambue kuwa yupo chini ya laana.

Utakapogundua kuwa kila unapotaka kupata upenyo unajikuta unarudi nyuma, fahamu kuwa uko chini ya mashambulizi makubwa sana ya shetani! Siku zote shetani hataki watu wafanikiwe bali waishi kwa mateso.

Eneo lingine ni ugonjwa wa ulimi. Wanawake wengi sana wanashambuliwa sana kupitia kinywa. Ni wepesi sana kuongea mambo ambayo hawaruhusiwi kuongea na mwisho hujikuta wakijiingiza katika matatizo makubwa.

Pasipo wao kujua, wamejikuta wakitoa siri zao kwa maadui zao. Ana wazo zuri la biashara, badala ya kulifanyia kazi kimya kimya, anatoa mipango yake kwa adui. Matokeo yake adui anamzunguka anampa ushauri mbaya.

Adui anaweza kumshawishi waingie ubia, wafanye biashara pamoja kumbe lengo ni kumfilisi mwishoni. Atamshauri achukua mkopo mkubwa huku akijua hataweza kuurejesha, hivyo kumuingiza kwenye madeni yasiyiolipika.

Mbinu nyingine ni misingi mibaya ya ndoa. Shetani ameunganisha wanawake wengi wenye neema kubwa kuolewa na wanaume wenye mapungufu au udhaifu mkubwa!

Hapa anachofanya shetani ni kuwaunganisha wanawake wachumbiwe na kuolewa na wanaume waliopagawa na mapepo(roho mbalimbali), hivyo kuharibu hatma zao.

Pia shetani amepindisha hatma za wanawake wengi kwa kuwafanya waolewe na watu wasio sahihi. Anakulengesha kuolewa na mwanaume mliokutana kwenye sherehe za harusi, kwenye sehemu za starehe, kumbe hakuwa sahihi.

Mbinu nyingine ni kuunganishwa na wakwe waliopagawa na mapepo. Wapo wakwe ambao ni washirikina wanawaloga hata wakamwana wao na hata wajukuu. Hawa hawajali kumpoteza mwana familia kwa kuwa ni maajenti wa shetani.

Wakwe wengi wamevuruga ndoa za wanawake kwa njia mbalimbali. Tena kama hajakupenda ndio kabisa atahakikisha anakuvuruga ukate tamaa na kuamua kuikimbia ndoa yako. Mwingine anahakikisha huzai ili iwe sababu ya kuondoka mwenyewe. Kumbe amehusika kukufunga uzazi.

Hasira ni roho nyingine anayotumia shetani kumvuruga mwanamke. Wanawake wenye roho hii au tabia ya hasira huwa wanateseka sana katika mikono ya shetani. Adui anatumia roho ya hasira kama njia ya kukuletea kila aina ya matatizo katika maisha yako.

Njia nyingine ni kukushambulia kwenye ndoto. Adui amejitahidi kushambulia maisha ya ndoto kwa wanawake wengi. Anawaletea kila aina ya ndoto chafu na kuwafanya wachanganyikiwe na kuleta huzuni kubwa sana katika maisha yao!

Shetani pia huwalengesha wanawake katika kila aina ya uovu kama vile uzinzi, uashetati na uchafu mwingine kuwakandamiza na kuwafanya kuwa wafungwa wa dhambi hiyo.

Isitoshe, shetani amepandikiza kila aina ya wanawake katika jamii zetu ili kuwatumia wavuruge ndoa za wanawake walio wengi. Nguvu za wanawake hawa (kahaba wa kuzimu) zimeumiza wanawake wengi sana kiroho, zimewaumiza mioyo kwa kuchezea hisia zao, akili zao na hata miili yao!

Jiulize, je, wewe ni mmoja wa wale waliolengwa kuvurugwa na shetani? Unahitaji kuomba sana! Hizi hapa mbinu jinsi ya kushinda mashambulizi haya.

Kwanza unapaswa kuungama dhambi zako na kuziacha kabisa. Kama hautatubu, shetani ataendelea kufanya uovu wake ndani ya maisha yako. Unatakiwa kuwa mbali na dhambi na kumkabidhi Mungu maisha yako!

Pili, hakikisha shetani hakudai chochote. Au una jambo lolote ambalo litaweza kumfanya shetani apate nafasi ya kukusumbua na kukushambulia.

Tatu, fanya maombi ya vita hadi uone vipo vitu vimeanza kubadilika katika maisha yako. Maombi ni nguvu, unapoomba unawasiliana na Mungu moja kwa moja kwani anakusikiliza.

**Anasema: "Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza". (Yeremia 29:12). Hadi wiki ijayo. Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Biteko anza na kilio hiki cha watoto maskini

HIVI unajua kadri unavyozidi kujitambua kuna watu unawakwaza? Unajua kwamba unachopaswa kukifanya ni kuchagua kuwakwaza au kuacha ndoto zako zipotee?

Wako Watanzania bado hawajajua wafanye nini wanapoona ndoto zao zinafifia au kuishia njiani.

Kuna jambo huwa linatatiza na sijui kama mamlaka za serikali zimewahi kubaini na kufikiria kuja na suluhu ya jambo lenyewe. Jambo lenyewe ni kuhusiana na dhana nzima ya masuala ya ajira na kukuza ujuzi.

Wanaokumbuka watanisahihisha. Serikali ilianzisha rasmi mafunzo ya uanagenzi mwaka 2016, ambayo hivi sasa yanasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Yalianzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mwaka 2012, na baadae kutolewa Tangazo la Serikali Namba 153 la Mei 4, 2012.

Kwamba programu hiyo ya mafunzo ya uanagenzi, itatoa fursa kwa kila mmoja kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kwa kuwa na ujuzi stahiki unaohitajika kufanya shughuli husika.

Mafunzo ya uanagenzi yanahusisha mhusika kutumia asilimia 40 ya muda wake kwa masomo ya nadharia darasani na asilimia 60 ya muda wake kwa masomo ya vitendo sehemu ya kazi.

Kama ndivyo! Kila mwaka mafunzo ya uanagenzi yanayotolewa nchini kupitia programu ya kukuza ujuzi iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, ikilenga zaidi kufungua fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Kila mwaka mafunzo haya ya uanagenzi yanatajwa kutafuna Sh. bilioni tisa ili kugharamia programu hiyo.

Kanzidata ya serikali inaonyesha kwamba mpaka kufikia sasa, zaidi ya vijana 130,000 nchini, wamenufaika na programu hiyo ya miezi sita.

Hasa kwa wale wanaojishughulisha na ufundi umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, useremala, ufundi magari, umeme wa magari, uchomeleaji na uungaji vyuma kwa waliopo kazini.

Wengine ni wale wa fani za utengenezaji wa vifaa vya aluminium, upishi, uhudumu wa hoteli na vinywaji, ushonaji, uchenjuaji wa madini, ufundi bomba, ufundi uashi, uwekaji wa terazo na marumaru, ufundi viyoyozi na majokofu.

Nimeandika waraka huu kwa sababu kuna kilio kikubwa huko kwenye vyuo. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Mashaka Biteko, anza na kilio hiki cha watoto masikini wanaotaabika kwa kukosa pesa za kujikimu.

Wanalia, wazazi wao au walezi wao hawana uchumi unaoweza kuwasaidia kufikia malengo yao.

Unapoingia kazini kuanza jukumu lako ulilopewa na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan la kuratibu shughuli za serikali na hili nalo uwe nalo akilini mwako.

Mshauri Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kuhusu hili na kama ikiwapendeza mlipe kipaumbele na tuone mabadiliko ya bajeti ya programu hii Bunge lijalo la bajeti.

Kwanza, niishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuendelea kutoa fursa hiyo kwa vijana.

Lakini, moja ya matatizo yaliopo katika utekelezaji wa programu hiyo ni vijana kushindwa kumudu gharama za maisha, ikiwamo chakula na malazi wanapokuwa chuoni.

Wako wanaosema pamoja na ada kulipwa au kugharamiwa na serikali, wapo vijana wanaoshindwa kuendelea na mafunzo na kuishia njiani kutokana na kushindwa kujikimu kimaisha.

Tunafahamu nia njema ya serikali ya kuwasaidia vijana, lakini ukitazama kwa kina kile kinachotolewa kwa kila kijana yaani bajeti, unatamani angalau kiongezwe kidogo kama kuna uwezekano.

Hii itawasaidia vijana waweze kumudu gharama za maisha kutokana na wengi kushindwa kumudu gharama za maisha ikiwemo chakula na malazi.

Hata ukiwasikiliza wanufaika wenyewe, utabaini kwamba serikali ina kazi nyingine ya kuwapatia mkopo kama makundi mengine ya jamii wanapomaliza kozi hizo ili waweze kujiajiri wenyewe.

Sote tunaamini nia njema ya serikali ya awali ya kuamua kukaa pamoja na waajiri, wakakubaliana kuwa ni lazima kuwe na programu ya taifa, ambayo itahusika kukuza ujuzi kwa vijana ili waweze kujiajiri na kuajiriwa.


Kimsingi, programu hii imejikita katika maeneo makuu manne, ambayo ni mafunzo kwa njia ya vitendo, kurasimisha ujuzi mahali pa kazi, mafunzo ya utarajali (internship) na kukuza ujuzi kwa waliopo kazini, kulingana na mabadiliko ya teknolojia."

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kwa mwaka wa fedha 2023/24, tayari serikali imetenga kiasi hicho cha fedha na kuanzia Julai imeshatoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Hata rehema za Mwenyenzi Mungu huwa hazichelewi, wala haziwahi. Hufika kwa wakati wake. Usichoke kusubiri, usikate tamaa mwishowe ukakufuru!

*** Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**







Kupendeza kwa Bi harusi kunatokana na ufanisi wa watu wawili muhimu ambao ni mpambaji na mrembaji. Pichani ni baadhi ya maharusi waliopata mwonekano mzuri baada ya kurembwa vizuri.

## MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# MAJIRA YA JOTO HAYOO

2023 umekuwa mwaka unaoshuhudiwa maendeleo ya kasi katika tasnia ya ubunifu wa mavazi.

Mavazi ya kitamaduni, vitambaa, jeanz na nguo za michezo yamezidi kuboreshwa na kuwavutia zaidi watumiaji.

Katika kipindi cha joto kinachotarajiwa kuingia mavazi hayo yatazidi kutawala na kuwanogesha watu kila mahali.

Ni wazi nguo za khanga, vitenge, suruali za vitambaa na vikoi zitazidi kuvaliwa kwa wingi kutokana na kuibuka mitindo mipya inayovutia.

Vazi la kaptula litashika nafasi zaidi na kufanya kampuni nyingi kubuni aina mpya ya mitindo.

Mchanganyiko wa vazi la blazer na suruali za kawaida nazo zitatamba na kuwafanya watu kuwa na machaguo mengi ya kutoka.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# TUNZA NGOZI YA MAFUTA

NGOZI yenye mafuta kwa kawaida huwa inang'aa, nene na yenye rangi iliyofifia.

Mara nyingi ngozi yenye mafuta mengi huwa na chunusi nyingi na vipelepele vyenye vichwa vyeusi.

Aina hizi za ngozi hutokana na tezi inayofahamika kama sebaceous ambayo inazalisha mafuta zaidi ya kiwango kinachotakiwa.Mafuta hayo husambaa katika ngozi na kuifanya iwe na unyevunyevu uliozidi.

**Namna ya kutunza ngozi**

Faida kubwa ya kuwa na ngozi yenye mafuta ni kwamba haizeeki haraka ikilinganishwa na aina nyinginezo za ngozi.

Miongoni mwa mambo yanayosaidia kuitunza ngozi yenye mafuta na kuepukana na chunusi ni yafuatayo.

Ngozi yenye mafuta inahitajika kusafishwa vyema kwa maji ya moto na sabuni ili kuzuia vinyweleo visizibwe na mafuta.

Epusha vifaa vigumu visikwaruze uso wako na kupelekea ngozi kubanduka, kwani suala hilo husababisha tezi za mafuta kufanya kazi zaidi ili kujaza sehemu iliyopotea ya mafuta.

Epuka kutumia vipodozi ambavyo huifanya ngozi yako ipoteze maji au kukauka. Matumizi hayo husababisha sehemu ya juu ya ngozi inyauke, na hivyo mafuta kuziba vinyweleo na kutokea vichwa vyeusi.

Jitahidi kuitunza vyema ngozi yako na kuisafisha vizuri. Jaribu kuosha uso mara mbili au tatu kwa siku.

Usioshe mara nyingi kwani kufanya hivyo huufanya uso kutoa mafuta zaidi.


Chagua kile unachosafishia kwa makini, jiepushe kutumia cream nzito au vifaa vigumu wakati wa kuosha uso wako.


Ni bora utumie sabuni za kawaida zisizokuwa na kemikali, unaweza kutumia kilainishi ngozi (lotion) ya kuua bacteria au sabuni zisizo na dawa nyingi.

Ni bora usioshe au kutumia losheni au mchanganyiko wenye alkoholi.

Tumia maji ya moto au ya vuguvugu wakati unaosha uso wako.







MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Supu ya utumbo wa ng'ombe

SUPU ya utumbo wa ng'ombe ni maarufu nchini, huliwa wakati wowote kutokana na ladha yake tamu.

Kwa kawaida supu ya utumbo hupikwa kwa kutumia utumbo wa ng'ombe uliosafishwa vizuri na kuchemshwa pamoja na mboga, viungo na nyanya.

**Mahitaji**

Utumbo wa ng'ombe nusu kilo, mashina ya giligilani, chumvi kijiko cha chai, pilipili manga kijiko cha chai, malimao mawili, mafuta vijiko viwili, kitunguu maji kikubwa kimoja na vitunguu swaumu kijiko cha chai cha vitunguu swaumu.

Majani ya figiri nusu kikombe, pilipili hoho moja, nyanya sita, oregano ya unga robo kijiko cha chai, tomato sauce nusu kikombe, viazi mviringo na karoti moja kubwa.



**MAANDALIZI**

Chukua utumbo na uondoe mafuta yote, kisha osha utumbo huo vizuri kwa maji safi yanayo tiririka.

Chukua sufuria kubwa, weka ndani ya hilo sufuria utumbo wa ng'ombe, majani ya giligilani, chumvi, pilipili manga, limao pamoja na lita mbili ya maji, kisha chemsha kwenye jiko lenye moto wa wastani, kwa muda wa saa 1 hadi 3.

Au kwa muda wa dakika 30 hadi dakika 60 kwa kutumia majiko yenye nguvu.

Maji yakipungua kumbuka kuongeza kadiri yatakavyoisha hadi utakapoona utumbo umeiva.

Utumbo ukishaiva, epua na uweke pembeni hadi upoe, kisha ondoa utumbo ndani ya sufuria na ukate katika vipande vidogo vidogo.

Chukua sufuria nyingine kubwa na uliweke kwenye jiko lenye moto wa wastani.

Weka mafuta ya kupikia ndani ya hilo sufuria, kisha acha mafuta hayo yapate moto. Weka vitunguu maji na ukaange hadi utakapo ona vitunguu hivyo vimebadilika rangi na kuwa vyeupe.

Weka majani ya figili, pilipili hoho pamoja na nyanya, kisha kaanga kwa dakika kadhaa. Weka oregano pamoja na tomato sauce, halafu koroga vizuri.

Weka utumbo, karoti na viazi mviringo, kisha acha vichemke kwa dakika kadhaa huku ukikoroga mara kwa mara.

Weka vikombe 3 vya maji pamoja na chumvi, kisha funika na acha ichemke katika moto mdogo kwa muda wa dakika 15, au hadi utakapoona viazi pamoja na karoti vimeiva. Supu imimine kwenye bakuli, tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# ZINGATIA MPANGILIO CHUMBA CHAKO

UMARIDADI huficha umasikini. Huu ni msemo wa siku nyingi tangu enzi na enzi unaotumiwa na wahenga wa lugha ya Kiswahili.

Umaridadi ambao tumeuzoea sana ni ule wa umahiri wa kujiweka safi katika uvaaji au kwa lugha ya kigeni 'smart' wakati wote bila kujali una kipato kikubwa ama la. Lakini leo nataka nikuambie kwamba pia umaridadi huo hufanywa hata katika nyumba.

Wengi wetu tumejikuta tukifanya chumba cha kulala kama sehemu ya kurundika vitu hovyo eti kwa sababu hapaonekani katika uso wa wageni kama ilivyo katika sebule. Chumba nacho kinapaswa kupangiliwa vizuri kama ilivyo kwa sebule au sehemu nyingine ya nyumba.

Kuna vitu muhimu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa ndani ya chumba ili kukifanya chenye mvuto, chenye afya na hata kuimarisha ustawi wa nyumba yako.

Moja ya vitu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa katika kukiweka chumba chako katika hali nzuri kwanza ni mpangilio wake hasa kwa kuangalia ukubwa na namna kilivyotengenezwa.

Zingatia kuweka vitu ambavyo ni muhimu na vina kazi na si kuweka kila kitu kwa sababu ukiweka vitu vingi ambavyo havina umuhimu kitakosa hewa na kitapoteza mvuto.

Mbali na hivyo, chumba kinachokosa mpangilio mzuri, uwezekano wa kukifanyia usafi wa uhakika ni mdogo na kwa maana hiyo hatari ya kuhifadhi wadudu ni kubwa.

Hakikisha samani muhimu pekee ndio zinawekwa ndani na zinafanyiwa usafi mara kwa mara.

Kwa kitanda, zingatia kukifanyia usafi kila siku, siyo kutandika mashuka tu lakini kuhakikisha unakikagua kila eneo na kufuta kabla ya kutandika shuka zako.


Kama kuna kabati, nalo uweke ndani yake vitu vinavyotumika pekee na kuvipangilia vizuri, ili liwe 'smart' na lisiharibu mpangilio wa chumba. Usiache kulisafisha kila mara.

Hakikisha nguo zako unazipangilia vizuri katika sehemu zake na viatu sehemu yake kwa kabati zenye sehemu ya kuwekea viatu hivyo.

Kwa upande wa 'dressing table', kama ipo, nayo vile vile inahitaji kuwa katika mpangilio mzuri, hakikisha vitu vinavyowekwa kwayo vinakuwa katika mpangilio mzuri unaovutia.Ondoa kila kitu ambacho hakistahili kuwekwa hapo na uwe unalifanyia usafi kila mara.

Ukiwa na uhakika kwamba chumba chako umekifanyia usafi wa uhakika na kila kitu kimewekwa katika mpangilio mzuri, siyo vibaya kupuliza kwa mbali marashi ili kinukie kidogo.

Kumbuka kufungua madirisha ni muhimu ili kuingiza hewa asili na kisha kufunga baada ya kuingia hewa ya kutosha ili kuzuia wadudu wasiingie.



## Tumia njia hii kupanga jiko dogo



**Na Restuta James**

BAADHI ya wasomaji wa ukurasa huu wamenipigia simu kutaka kujua wanawezaje kuweka kila kitu cha msingi kwenye chumba kidogo cha jiko.

Wengine wamezungumzia changamoto wanazokutana nazo kwenye nyumba za kupanga, wamiliki wengi hawatilii maanani umuhimu wa jiko.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa hata jiko dogo, unaweza kupangilia vizuri na kuweka vitu vyote vya msingi.


Akizungumza na Nipashe mapema wiki hii, mtaalamu wa mpangilio wa nyumba na mapambo, Brown Joseph, anaeleza kuwa jambo la msingi ni kuhakikisha kila mita moja ya mraba inatumika ipasavyo.

Anasema mpangilio mzuri utalipa jiko mwonekano maridhawa na 'uficha' udogo wake wa asili.

1. Kama kuta za chumba hiki hazijabandikwa marumaru, hakikisha unapaka rangi ya kuvutia.
2. Nunua vyombo muhimu tu, kuanzia sufuria hadi sahani. Hii itakuepusha kuwa na vitu visivyotumika.
3. Buni kabati dogo linaloweza kukaa ukutani na kuhifadhi vyombo vichache ulivyonavyo.
4. Meza ya jiko isiwe pana sana, hii itakupa nafasi ya kuweka ua au mmea wa asili kama rosemary.
5. Waweza kuweka kabati dogo ukutani kwa ajili ya viungo vya chakula, hii itakupa nafasi ya kutembea ndani ya chumba hicho.

**Tuwasiliane kupitia 0753 33330, barua pepe restutajames@gmail.com**

# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
'MPE TALAKA MKEO UMJUE ALIYEKUWA ANAMPA KIBURI'
JUKWAANI
SIKU HIZI HATUITWI 'WAPIGA DEBE WA WANA-SIASA TUNAITWA CHAWA, TUNAFYONZA 'MAOKOTO' USHANISOMA?
HATA MKIJIITA 'KUNGUNI' TUTAWA-KUMBATIA
WEWE HUKO JIMU UNA LAKO JAMBO! KAMA KUPUNGUZA KITAMBI 'MBINU NDIO HIZI NINAZO' SEMA JINGINE
NSEMEJE WE'NIPASUE BANDAMA MGOMBEE MSIBA!
MIMI NA WEWE AKILI ZETU ZINAFANANA
WE! TEMEA MATE CHINI! SIJAWAHI KUHONGA MSHAHARA WOTE TOKA NIZALIWE
DALILI ZIKO WAZI KABISA MUDA WOWOTE LINAPIGWA JITU KAMA NGOMA YA MKOLE WA KIZARAMO
GARI TAYARI IMESIMAMA!
MKITAKA NGUMI ZA 'MSAGULANO' ANZENI KUPI-GANA HUMU!
MSAGULANO UNAMAANISHA UNACHAGUA KIBONDE
RUKSA PIGANENI ILA MVUNJANE MIFUPA YENU MSIVUNJE VIOO
HIYO IMEENDA!
MIAKA MINGI IMEPITA NI TUKIO GANI UNALIKUMBUKA ILE SIKU YA HARUSI YETU?
ZILIPOKUKOLEA UKAMUITA BABA MKWE WAKO 'WIFI'
UNGESEMA VINGINE USHANIHARIBIA NDOA MWENZAKO JAMANI OHOOO NAFA MIE!
LAKINI BOSI KWANI UONGO SIJAKUSHUSHA 'GESTI' ILI UPUMZIKE VIZURI KWA KUWA MKEO ANA GUBU?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KAZI UKWENI MSHAHARA 'ASANTE'

## HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis aionya Mongolia kuhusu kukithiri kwa rushwa

**ULAANBAATAR,** MONGOLIA
KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis amesifu busara za watu wa Mongolia kwa kudumisha amani na ustahimilivu wa kidini.

Papa Francis aliitahadharisha nchi hiyo juu ya vitendo vya rushwa na uharibifu wa mazingira.

Kiongozi huyo mwenye miaka 86, aliyasema hayo katika ziara yake ya siku tatu nchini Mongolia iliyoanza Ijumaa na alikaribishwa kwa sherehe rasmi iliyokuwa na gwaride la wapanda farasi mbele ya Kasri la serikali.

Akiwa nchini humo alikutana na Rais Ukhnaagiin Khuresukh na kutia saini kitabu cha wageni na kuandika kwamba anatembelea taifa hilo changa lenye historia kongwe la kisasa na lenye utajiri wa tamaduni.

Papa Francis ameitembelea nchi hiyo yenye idadi ndogo zaidi ya waumini wa dhehebu la Kikatoliki duniani ikiwa na wafuasi 1,450.

Awali aliusalimu umati wa watu waliokuwa wamesimama mbele ya sanamu la shaba la Gengis Khan huku vijana wa kikatoliki wakimshangilia.

Safari hiyo pia imewavuta waumini wa Kikatoliki kutoka nchini China ambao walihudhuria pia hafla ya kumkaribisha Papa.

Ziara hiyo ya kidiplomasia ya Papa Francis inalenga kutafuta mshirika asiye na upande wowote, wakati Vatican ikifanya juhudi za kuimarisha uhusiano wake na Mongolia pamoja na mataifa jirani.

Kiongozi huyo alisema, utamaduni wa Washamani na waumini wa Buddha wa kuishi kwa amani na mazingira pamoja na viumbe vilivyomo ndani yake kunaweza kuchangia juhudi za kuinusuru na kuihifadhi sayari ya dunia.

Pamoja na Papa Francis kuipongeza Mongolia, pia alionya dini inaweza kusaidia kujilinda dhidi ya kitisho cha rushwa ambacho ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii.

Aliongeza kuwa serikali hazina sababu ya kulihofia kanisa katoliki kwani halina ajenda yoyote ya kisiasa.

Mji wake mkuu wa Ulaanbaatar ni moja kati ya miji yenye kiwango kibaya zaidi cha uchafuzi wa hali ya hewa.

Maofisa wa serikali walikuwa wakituhumiwa kwa vitendo vya rushwa hali iliyosababisha kuzuka kwa maandamano mwaka uliopita.

Sehemu kubwa ya nchi hiyo pia iko hatarini kuwa jangwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi, uchimbaji madini na kulisha mifugo mingi kupita kiasi katika baadhi ya maeneo.

Ziara ya Papa Francis inadhamiria pia kupeleka ujumbe wa kanisa kwa maeneo ya mbali na yasiyopewa kipaumbele.

**DW**



Papa Francis akisalimiana na waumini wa kanisa Katoliki wakati akiwa katika ziara yake nchini Mongolia. **PICHA: DW**

# India yarusha chombo kutafiti jua

**MUMBAY,** INDIA
INDIA imerusha chombo cha anga za mbali kitakachokwenda kulifanyia utafiti jua, wiki mbili tangu ilipofanikiwa kutuma chombo kingine mwezini.

Roketi iliyobeba chombo hicho cha utafiti katika jua kilichopewa jina la Aditya-L1, iliruka mapema jana alfajiri kuanza safari ya kiasi umbali wa kilometa milioni 1.5 kutoka sayari ya dunia.

Shirika la Utafiti wa Anga za Juu ya India, limesema chombo hicho kitatafiti tabaka la juu la Jua, maumbile na upepo kwenye nyota hiyo muhimu katika mfumo wa sayari unaoijumuisha dunia.

Hatua hiyo inafuatia mafanikio ya waliyopata mnamo Agosti 23, baada ya India kuwa taifa la kwanza duniani kupeleka chombo kwenye ncha ya kusini ya mwezi.

Utafiti kuhusu Jua na mafanikio ya kutuma chombo mwezini kunaimarisha nafasi ya India katika shughuli za utafiti wa anga za juu duniani.

**DW**

# Kiongozi upinzani Senegal amaliza mgomo wa kula

**DAKAR,** SENEGAL
KIONGOZI wa upinzani nchini Senegal, Ousmane Sonko, ambaye yuko kizuizini, amemaliza mgomo wa kula uliodumu kwa muda wa mwezi mmoja.

Sonko ambaye ameweka nia ya kuwania kiti cha urais akiwa mpinzani wa Rais Macky Sall, amekuwa akikabiliwa na msururu wa mashtaka tangu 2021.

Bamba Cisse, mmoja wa mawakili wake alithibitisha kiongozi huyo kuwa amemaliza mgomo huo.

“Ousmane Sonko amefuta mgomo wake wa kula,” alisema msemaji wa chama chake, El Hadji Malick Ndiaye, kwenye mtandao wa Facebook na ule wa X. Kwa mujibu wa mawakili wake, baada ya kuanza mgomo huo, Sonko alilazwa hospitalini na baadaye kulazwa katika chumba cha wagonjwa mahututi. Mawakili wake walionya kuwa hali yake ya kiafya inazidi kuwa mbaya na kuwa maisha yake yamo hatarini.

Sonko alikamatwa mwishoni mwa mwezi Julai na kushtakiwa kwa uhalifu ikiwa ni pamoja na kuanzisha uasi, uhalifu wa kujihusisha na mtandao wa kigaidi na kudhoofisha usalama wa serikali.

# Ukraine yakiri kushambulia kambi ya kijeshi Russia

**KYIV,** UKRAINE
UKRAINE imethibitisha kuwa ndege zake zisizo na rubani zilirushwa na kushambulia uwanja wa ndege wa kijeshi wa Pskov nchini Russia.

Shambulizi hilo lilifanyika usiku wa kuamkia Jumatano ya wiki hii.

Akihojiwa na jarida maalumu la The War Zone, mkuu wa ujasusi wa kijeshi wa Ukraine Kyrylo Boudanov, alithibitisha kuwa ndege hizo hazikurushwa kutoka Ukraine, badala yake zilikuwa eneo la Russia.

“Ndege zisizo na rubani zilizotumiwa kushambulia kambi ya anga ya Kresty huko Pskov zilirushwa kutoka ndani ya Urusi,” alisema.

Ofisa huyo alikataa kutaja ikiwa shambulio hilo lilifanywa na vijana wake au Warussia wanaofanya kazi kwa niaba ya Ukraine.

Hata hivyo, jarida hilo lilichunguza picha iliyopigwa na moja ya ndege zisizo na rubani, lilikadiria kuwa waliofanya shambulio hilo walikuwa karibu na kambi hiyo ya kijeshi.

Kwa mujibu wa The War Zone, ndege zisizo na rubani zilizotumika hazikuwa kamikaze, lakini zilikuwa na uwezo wa kurusha mabomu madogo.

Kwa mara ya kwanza Ukraine inakiri kutekeleza mashambulizi katika ardhi ya Russia.

**RFI**

MAKALA

# ARUSHA DC IMETEGUA KITENDAWILI SAMARIA



Na Magabilo Masambu

KUNA baadhi ya watu huwa wanasema Tanzania wakati fulani ilikuwa inafanana kimaendeleo na baadhi ya nchi kama China, Singapore na Korea Kusini lakini wanashangaa kwa nini nchi hizo zimepiga hatua kuishinda Tanzania. Kuna hotuba moja ya Mwasisi wa Taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere alipokuwa anaeleza China itakavyoweza kuja kuwa taifa kubwa kiuchumi duniani kama tunavyoona sasa.

Mwalimu anaeleza kitu alichokiona wakati ameitembelea China miaka ya 1960 akasema kilichomshangaza wakati huo ni kuona Wachina wakizalisha bidhaa za kibiashara huku wakiwa kwenye majengo yenye vumbi yasiyo na sakafu na wakati mwingine yametoboka katika mapaa. Hiyo haikuwafanya wakate tamaa bali wakawa wanazalisha bidhaa bora kabisa. Kitendo hicho kilifanya Mwalimu awe na matumaini kwamba siku za usoni China itakuwa na nguvu kiuchumi na leo tunashuhudia.

Ninachotaka kusema ni kwamba katika kuyatafuta maendeleo ni muhimu kuwekeza zaidi katika vitendelea kazi, ili baadaye vizae majengo mazuri. China hawakuanza kuwekeza kwenye majengo mazuri bali waliwekeza kwenye vifaa vya kuzalishia kwa maana ya viwandani na leo wana majengo mazuri ya mfano.

Wakazi wa Samaria na Halmashauri ya Arusha wameamua kufanya ya China kwa kutumia rasilimali walizo nazo katika soko jipya na kutegua kitendawili cha muda mrefu. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Ojung'u Salekwa, amezindua soko la Samaria katika kijiji cha Samaria kata ya Nduruma. Hafla ya uzinduzi imefanyika katika viwanja vya soko hilo, wananchi na wafanyabiashara katika eneo hilo wamejitokeza kwa wingi kuonyesha walikuwa na uhitaji wa muda mrefu.

Salekwa amewapongeza wananchi wa Samaria na vijiji vya jirani kwa ushirikiano na uzalendo walioonyesha, tangu kuasisiwa kwa wazo la kuwa na soko mwaka 2008 na hatimaye mwaka huu wa 2023 wazo limekuwa halisi.

"Niwapongeze sana wananchi wa hapa Samaria na viunga vya jirani haikuwa rahisi. Kuwa na soko hapa, kutawezesha sasa akina mama kutosafiri tena umbali mrefu, jambo lililowafanya wakati mwingine muamke saa nane za usiku, kuwahi kwenye masoko mengine kama Samunge, Tengeru na sehemu nyigine. Sisi kama Serikali na halmashauri kwa ujumla, tutaendelea kuhakikisha huduma za msingi zinapatikana ili kurahisisha ufanyikaji mzuri wa biashara. Changamoto zilizobaki ndogo ndogo tutazishughulikia, ili soko liweze kuhudumia Arusha nzima na wilaya za jirani," anasema.

Hata hivyo, Diwani wa Nduruma, Raymond Stephano, amesema lengo kuu la kuanzisha soko hilo katika kata yake ni kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi.

"Tunahitaji kuona wananchi wetu wanakua kiuchumi, lakini soko hili litakuwa mwarobaini kwa wakulima wa mboga mboga, ambao huwa wanateseka sana kusafirisha mazao yao ya bustani hadi Samunge, zaidi limerahisisha wakazi wa hapa na jirani kujipatia mahitaji muhimu kwa karibu."

Sophia Mollel, mama mwenye kibanda anayefanya biashara sokoni hapo, ameupongeza uongozi wao wa kijiji kwa kushirikiana na wananchi, mpaka kuhakikisha sasa wanafanya biashara hapo.

"Mimi nilikuwa barabarani, nimekuja nikapewa eneo bure na sasa kama unavyoona tumefungiwa mpaka taa za umeme, maji unayaona yanatoka mengi tu hapo bombani, kwahiyo kwakweli tunaishukuru serikali hasa sisi akina mama, tutaweza kufanya biashara kwa utulivu na kuweza kupata chochote kitu," anasema.

Akiwasilisha taarifa yake kwa niaba ya wanakijiji wa Samaria mbele ya mgeni rasmi, Upendo Daudi Mangusha, ameweka wazi kuwa soko hilo ni la kila siku kwa wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo lakini kila Alhamis ya juma, kutakuwa na gulio kwa ajili ya wananchi wote wa wilaya ya Arusha na mkoa mzima.

Mwenyekiti wa soko hilo, Lairivani Mollel, anaeleza mchakato ulivyokuwa kiasi cha jambo hilo kuchukua muda mrefu bila wakazi wa Samaria kupata soko.

"Kwanza katika ubunifu wake mimi nilikuwa mjumbe wa serikali ya kijiji kwa kipindi hicho, wakati wa kupendekeza kwamba soko liwe pale palitokea mabishano sana miongoni mwetu, lakini mwisho wa yote leo tumepata soko, namna tulivyofanya tulikuwa tunawapatia watu vizimba bure. Kwa hiyo wengi wakajitokeza na tukawashauri watumie tu vitu vilivyopatika kwa urahisi kama miti kujenga na sasa unaona soko limependeza. Kabla ya hapa, tulikuwa zaidi tukitegemea soko la Olokii ambako kuna wakati mto ulikuwa ukijaa tunashindwa kuvuka na hivyo kushindwa kufanya biashara, lakini leo hii hata kama mvua itanyesha biashara itafanyika vizuri kabisa", anasema.

Samaria ni miongoni mwa vijiji vinne vinavyounda kata ya Nduruma, katika tarafa ya Moshono, halmashauri ya Arusha mkoani Arusha. Ujenzi wa masoko umeendelea katika maeneo mbalimbali ya nchi katika kuleta huduma karibu na wananchi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa cha mwenye nyumba dowezi kwa wake za wapangaji*



Na Adam Fungamwango

UMESHAWAHI kukutana na baba mwenye nyumba mtata, au mama mwenye nyumba mcharuko? Usiombe yakukute kwani wakati mwingine wanaoishi nyumba za kupanga wanakutana na madhila mbalimbali ya kusikitisha na kushangaza.

Baadhi ya wenye nyumba wanawachukulia wapangaji wao kama sehemu ya familia yao. Amri na masharti yote atakayoyaweka basi yanatakiwa yafuatwe mbali kabisa ya yale yaliyomo kwenye mkataba.

Wachoshindwa kufahamu ni kwamba mpangaji ametoa pesa yake ya kodi, hivyo ana haki ya kuishi anavyotaka yeye mradi tu havunji masharti ya mkataba.

Unaweza kukuta mwenye nyumba hataki wageni nyumbani na wapo hasa mama wenye nyumba wanaweza kupangia wapangaji wao hata watu wa kuongea nao. Wengine marufuku. Mpangaji anakuwa hana uhuru kana kwamba yuko jela. Wengine wana gubu, kila kinachofanywa na mpangaji yeye anapinga tu.

Kuna kisa kimoja kimesimuliwa na bendi ya Super Matimila katika kibao chao kinachoitwa 'Nyumba za Kupanga' lakini maarufu kama 'Hamisa.'

Ni wimbo unaomzungumzia baba mwenye nyumba mmoja ambaye hakai hapo, lakini huja mara kwa mara kuzungukia wapangaji wake.

Baba huyo ana tabia ya kutongoza wake za wapangaji wake hasa wale wapya ambao wamepanga si muda mrefu uliopita.

Wimbo huu ulirekodiwa kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) mwaka 1991, utunzi wake Dk. Remmy Ongalla. Yeye mwenyewe akikamata gita la solo na kuimba akishirikiana na Roshy Mselela, Cosmas Chidumule na mwanamama Hamisa Hamisi.

Gita la rhythm lilipigwa na Mjusi Shemboza, gita la besi likaungurumishwa na Muhidini Kisukari, Lawrence Chuki alikuwa kwenye drums, na tumba zilipigwa na Idd Yusuph.

Wimbo huu unazungumzia madhila na vituko vinavyoweza kutokea kwenye nyumba za kupanga.

Dk. Remmy anakutana na binti mmoja mrembo mkoani anaitwa Hamisa, pamoja na kumwambia anampenda lakini anaogopa kumhamishia Dar es Salaam akidai kuna manyanyaso na vituko kwa baadhi ya wenye nyumba na mashairi ya wimbo huo yanaanza hivi.

"Hamisa eee, Hamisa eee, Hamisa eee, Hamisa ee, nimetokea kumpenda Hamisa wewe Hamisa, Hamisa mtoto wa Kigogo Hamisa wee, Hamisa umezaliwa Mpwapwa, pia waishi Dodoma, kila nikifikiria Hamisa nikuhamishie Dar es Salaam lakini naogopa Hamisa we.

Dar es Salaam kuna vituko, watu twaishi nyumba za kupanga, wenye majumba hutunyanyasa Dar es Salaam, Hamisa ooo, Hamisa."

Baada ya kipande hicho, kinafuatia kipande cha maigizo au majibizano ya Baba mwenye nyumba na mke wa mpangaji wake katika kuthibitisha kile ambacho amekibainisha.

Dk. Remmy mwenyewe ndiye anayeigiza au kuongea kama baba mwenye nyumba na mwimbaji wa kike wa bendi hiyo wakati huo, Hamisa Hamisi anacheza kama mke wa mpangaji.

Kipande hicho kinaonyesha kuwa baba mwenye nyumba ametoka anakoishi na kutembelea nyumba yake aliyoipangisha.

**Mwenye nyumba:** Hodi hodi hodi hodi huku jamani hodii

**Mke wa mpangaji:** Karibu!

**Mwenye nyumba:** We mke wa nani katika nyumba hii?

**Mke wa mpangaji:** Mi mke wa fundi koroboi hapo miembeni.

**Mwenye nyumba:** Mwenye anaishi katika banda la uani huku?

**Mke wa mpangaji:** Mmmmm! (anaitikia)

**Mwenye nyumba:** Bwana 'ako kaenda wapi?

**Mke wa mpangaji:** Bwana 'angu kaenda Gerezani kutafuta makopo.

**Mwenye nyumba:** Atarudi saa ngapi?

**Mke wa mpangaji:** Atarudi saa sita.

**Mwenye nyumba:** Hivi we mtoto unanijua mimi ni nani?

**Mke wa mpangaji:** Hivi wewe ndiyo nani?

**Mwenye nyumba:** Mimi ndiyo mwenye nyumba hii.

**Mke wa mpangaji:** Mmmmmm! Shikamoo.

**Mwenye nyumba:** Marahaba marahaba.

**Mke wa mpangaji:** Karibu unywe chai.

**Mwenye nyumba:** Ahsante Ahsante, mpaka nikwambie kama mi' ndiyo mwenye nyumba hii ndiyo unaniamkia shikamoo, haya maharaba mama.

**Mwenye nyumba:** Sasa we mtoto umetokea wapi?

**Mke wa mpangaji:** Mimi nimetoka Mpwapwa.

**Mwenye nyumba:** Umetoka Mpwapwa

**Mke wa mpangaji:** Mmmmmm! (anaitikia)

**Mwenye nyumba:** We Mgogo?

**Mke wa mpangaji:** Aka, mi' siyo Mgogo, mi' Mkaguru.

**Mwenye nyumba:** Unajua we mtoto.

**Mke wa mpangaji:** Mmmmmm! (anaitikia)

**Mwenye nyumba:** Ukifika hapa Dar es Salaam lazima ungetuona watu kama sisi.

Ungepewa kila kitu bure, unasemaje au vipi?

**Mke wa mpangaji:** Basi nitamsubiri mume wangu akija nimuelezee eti tumepewa chumba cha bure.

**Mwenye nyumba:** (kwa hasira) Utamsubiri mume wako akija umwambie Mtumwaulete ametupa chumba cha bure!

**Mke wa mpangaji:** Eeeee

**Mwenye nyumba:** Basi akija umwabie fungasheni na ondokeni. Ondokeniii!

**Mke wa mpangaji :** Basi!

Hivi ni baadhi tu ya vituko vya wenye nyumba. Hapa tumeona baba mwenye nyumba akitumia udhaifu wa dada aliyetoka mkoani, akiolewa na mume ambaye hana nyumba na ana maisha duni.

Anatumia ubaba mwenyenyumba wake, mali yake ambayo ni nyumba kutaka kumshawishi binti wa watu ili amrubuni kimapenzi.

Waswahili wanasema ukishangaa ya Mussa utaona ya Firauni, haya ni maisha halisi ambayo yapo kwenye jamii yetu hasa 'uswahilini.'

Kwa bahati nzuri, wanamuziki wa zamani walikuwa wanapenda kuyachukua na kuyaweka hadharani kwa lengo la kuonya, kufundisha na kuburudisha.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie kwenu-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




DAKIKA 15 baadaye Catty alitoka chumbani. "Naona umeipenda hiyo tamthilia." Akamshtua.

Akatabasamu halafu akajibu. "Ni kweli nzuri sana ila mimi mara nyingi sina muda wa kuangalia sana haya mambo."

"Vipi huyu mwehu ameshatoka!"

"Kaondoka kapita kanuna utafikiri kalazimishwa kuolewa na mwanaume asiyempenda."

Catty akaangua kicheko. "Kha! usinichekeshe mie James, kumbe una maneno hivyo. Vipi alipoondoka alikwambia kitu gani?"

"Hapana, hajaniambie kitu chochote, katoka vimbisha domo tu hapa." Akaongopa.

Ni kweli alitoka amenuna, lakini James hakutaka kumwambia ndugu yake kuwa dada yake amemwambia 'Kafie kwenu.'

Pamoja na yote, James pia na busara. Hakutaka kuwagombanisha ndugu hao. Hakutaka wagombene kwa ajili yake. Yeye ni mtu wa kupita. Ni mpita njia, anasaidiwa kwa muda na siku si nyungi atarudie maisha yake. Hatofika tena pale. Kwa nini aondoke hapo na kuwaacha na ugomvi?

Alitaka wandelee kuwa na amani na undugu wao kama kawaida. Akajua yeye akiwa ndiyo sababu ya ugomvi wa ndugu hao, baadaye wote wanaweza kumchukia.

"Na yale aliyokuwa akiongea wakati mimi nimetoka?"

"Catty, si unamfahamu ndugu yako? Wewe acha tu, yeye anaongea mradi anajifurahisha, we unadhani mimi ndiyo kwanza nayasikia hayo maneno yake? Mimi hapa nimekufuata wewe mhisani wangu tu basi. Yeye na mimi tunamalizana wenyewe tu mbele ya safari huko."

"Ina maana bado hujamuacha tu na hamsini zake?"

"Unajua nataka kufanya nini Catty? Nataka nikae kimya kama mwezi mmoja, mmoja na nusu au miwili nimuingie tena, labda kichwa chake kinaweza kuwa kimetulia." Akajitutumua James.

Kauli hiyo ilimfanya Catty kuangua kicheko kikali. Kikamshangaza hata James mwenyewe.

"Vipi dada, mbona umecheka sana, unaonekana kufurahi namna hiyo?"

"Nacheka unavyojiamini! Napenda kujiamini kwako, lakini bado hujapata mtu."

"Una maana gani Catty?"

"Mimi nikwambie tu ukweli kama rafiki yako! Sitaki kupindishapindisha, Carry humuwezi na hutomuweza."

Moyo wa James ulikufa ganzi ghafla, akauliza swali.

"Kwa nini unasema hivyo Catty?"

"Mimi nakushauri uangalie utaratibu mwingine wa maisha."

" Catty, una maana gani?"

"Upande wa pili." James akabaki anamshangaa.

"Sijui umeelewa ninachomaanisha?"

"Hapana."

"Unampenda Carry, lakini kwa jinsi ninavyoongea naye, na yule ni ndugu yangu hanifichi chochote, hakupendi na wala hakuhitaji." Akanyamaza kwanza kumtazama jinsi uso wake ulivyosawijika.

James aliangua kicheko, ambacho hakijulikana kama ni cha furaha au huzuni.

"Kwa nini uteseke unaendelea kuumia na mtu asiyekupenda, amua moja kama mwanamume!"

Bado James alikuwa njia panda asijue ni kitu gani ambacho anatakiwa aamue.

"Lakini bado sijakata tamaa, anaweza kunielewa, mwanamume hatakiwi kukata tamaa, ndiyo maana vyote anavyofanya, na anavyoniambia na kunikwaza, mimi navivumilia, ipo siku atakuja kuelewa." James akajibu.

> **"Unajua nataka kufanya nini Catty? Nataka nikae kimya kama mwezi mmoja, mmoja na nusu au miwili nimuingie tena, labda kichwa chake kinaweza kuwa kimetulia." Akajitutumua James.**

Hapo ndipo Catty akatoa lile tabasamu lake kiasi cha mwanya wake aliojaaliwa na Mungu kuonekana.

"James, nimetoka kukwambia sasa hivi hapa kuwa yule ni dada yangu, ndugu yangu, tumepishana miaka miwili tu, tumekuwa wadogo pamoja, tumecheza pamoja, kwa hiyo kila mmoja anaijua tabia ya mwenzake. Wewe humjui yule, mimi ninayezungumza na wewe ndiyo najua alivyo. Kifupi tu kuwa hayo maneno unayoongea ni ya kujifariji tu na kujipa moyo! Haiwezekani!"

Maneno hayo yalimfanya kung'aa macho.

"Nikwambie haupo kwenye moyo wa Carry, kabisaaa, sikufichi."

"Sasa wewe ni ndugu yake, kwa nini usikae naye kumuleweshа, au kunisaidia? Wewe umenisaidia sana, halafu ni mkarimu kuliko ndugu yako, mnafanana kila kitu, sura muonekano, lakini tabia ni tofauti, wewe ni mkarimu mpole na mwelewa, ndugu yako ni mkali sana halafu mgumu mno kuelewa, naomba unisaidie, anaweza kukuelewa kwa sababu wewe ni ndugu yake."

Catty alimtazama kwa makini James, halafu akatikisa kichwa kuonyesha kumuonea huruma na pia hawezi kupata kitu chochote anachohitaji kutoka kwa ndugu yake Carry.

"Nipe ushauri basi Catty, nifanyeje mwenzako?"

"Sijui kama unaweza kuukubali ushauri wangu kwa sababu ni mgumu sana."

"Mgumu!?" Akauliza na kushangaa kwa wakati mmoja.

"Mgumu kama utashupaza shingo, lakini kama ukiufuata ni rahisi sana."

James akawa na hamu na haraka ya kutaka kuusikia ushauri huo ambao anataka kupewa na Catty, ndugu yake Carry.

"Usihangaike na mtu asiyekupenda siku zote. Carry ni sistaduu, anapenda mambo makubwa, anapenda maisha ya juu na vitu vya gharama, hawezi kuwa na mwanamume kama wewe, anataka wa hadhi ya juu wenye pesa, mali, vyeo, hadhi. Na siyo yeye tu, wasichana wengi wa kisasa ndivyo walivyo."

James alinyamaza kimya. Maneno yalikuwa yanamuingia na kuyaelewa, lakini bado akili yake bado ilimtuma kukataa.

"Tafuta wa saizi yako. Usipende kudhalilishwa na kila mwanamke unayekutana naye barabarani. Kuna wengine watakukataa kistaarabu, lakini wengine watakudhalilisha kama anavyokufanya dada yangu." Akaongezea nyundo nyingine.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# HAITHAM KIM UMEKWENDA, UTAKUMBUKWA KWA MENGI

MWIMBAJI wa Bongofleva Haitham Ghazal Seif, maarufu kama Haitham Kim, amezikwa katika makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam jana.

Shughuli ya mazishi ilihudhuriwa na wasanii mbalimbali na wadau wa muziki ambao walionekana kuwa na majonzi wakati jeneza lake likiwasili eneo la makaburini.

Kim alifariki Ijumaa katika Hospitali ya Rufaa ya Temeke baada ya kusumbuliwa na tatizo la upumuaji.

Akiwa hospitalini hapo, wasanii na wadau wengine walianzisha kampeni ya kuchangisha pesa kwa ajili ya kusaidia matibabu yake.

Mume wa marehemu, Bryson amesema hali ya Haitham ilibadilika ghafla siku saba zilizopita akisumbuliwa na upumuaji baada ya kupata homa ya kawaida.

Amesema Haitham alionekana kuzidiwa kwa kukosa pumzi na kuharakisha kumpeleka hospitali hiyo ambako aliwekewa mashine kumsaidia kupumua.

# TEKNO ATAMBULISHA ALBAMU MPYA

MWANAMUZIKI na mtunzi maarufu kutoka Nigeria, Tekno, amezindua albamu yake mpya 'The More The Better' ikiwa na nyimbo 13.

Albamu hiyo ni mwendelezo wa safari yake ya muziki, akianzia ile ya kwanza, Old Romance, ambayo aliitoa 2020 na baadhi ya nyimbo zilitamba kwenye chati za muziki.

Akitumia muziki aina ya Afrobeats, mafanikio yake yalianza kuonekana miaka ya 2010, baada ya kuandika historia ya kutoa nyimbo mfululizo zilizovuma duniani kote.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SALAH NA SAUDIA
KLABU ya Al-Ittihad iko tayari kutoa dau la pauni milioni 200 kwa ajili ya mshambuliaji wa Liverpool kutoka, Misri Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, kabla ya dirisha la usajili la Ligi ya Saudia kufungwa Septemba 7. **(Mail)**

### BAKAYOKO AWINDWA
LIVERPOOL tayari ina mbadala wa Mohamed Salah na huenda wakamnunua winga wa PSV Eindhoven raia wa Ubelgiji, Johan Bakayoko mwenye umri wa miaka 20 Januari ikiwa mshambuliaji huyo wa Misri ataamua kuondoka. **(Express)**

### MASON MAMBO MAGUMU
LAZIO iliamua kutomsajili mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 21 kabla ya kujiunga na Getafe kwa mkopo siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho. **(Goal)**

### HOJBJERG HAUZWI
MAZUNGUMZO ya Atletico Madrid na Tottenham Hotspur kumhusu kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28 yalimalizika baada ya Spurs kukataa ofa ya kwanza kwani haikujumuisha wajibu wa kununua. **(Fabrizio Romano)**

### ADAMS ALIZUIWA
KLABU ya Southampton ilizuia uhamisho wa mkopo wa mshambuliaji wa Scotland, Che Adams mwenye umri wa miaka 27 kwenda Wolves. **(Athletic)**

### DIRISHA GUMU
KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino amesema dirisha la usajili limekuwa "gumu" licha ya timu yake kutumia zaidi ya pauni milioni 360 msimu huu. **(FourFourTwo)**

### PEPE KUONDOKA
WINGA wa Ufaransa, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 28 anaweza kuondoka Arsenal na kuelekea Saudi Arabia katika klabu ambayo haijatajwa jina lake kabla ya dirisha la usajili la kufungwa Septemba 7. **(Football London via Fabrice Hawkins)**

### ARSENAL NA PEPE
KLABU ya Arsenal ilifikiria kusitisha mkataba wa Nicolas Pepe Ijumaa, mwaka mmoja kabla ya kumalizika kwa mkataba wake, baada ya mpango wa kuhamia Besiktas kushindwa. **(Mail)**

### GRAVENBERCH NAMBA NANE
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anatarajiwa kumpanga kiungo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 21 na mchezaji mpya Ryan Gravenberch katika nafasi ya namba nane. **(Express)**

### BAYERN ILIKOSA WATATU
KLABU ya Bayern Munich ilishindwa kulenga shabaha tatu katika siku ya mwisho ya uhamisho - kiungo wa Ureno, Joao Palhinha mwenye miaka 28, alibakiwa na Fulham , mlinzi wa kati wa Ujerumani, Armel Bella-Kotchap mwenye miaka 21, aliamua kuhamia kwa mkopo PSV Eindhoven kutoka Southampton na mlinzi wa Chelsea, Trevor Chalobah mwenye miaka 24, liyebakia Stamford Bridge. **(Goal)**

### DAKA ILISHINDIKANA
PENDEKEZO la Bournemouth la kutaka kumnunua mshambuliaji wa Leicester City na Zambia, Patson Daka mwenye umri wa miaka 24 halikufaulu katika saa za mwisho za dirisha. **(Goal)**

### FALL ATUA BARCA
MLINZI wa Senegal, Mamadou Fall mwenye umri wa miaka 20 alikamilisha uhamisho wa mkopo kutoka klabu ya Los Angeles FC kwenda Barcelona siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho, akiwa na chaguo la kufanya uhamisho wa kudumu wa pauni milioni 5.6

***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# JOAO FELIX, CANCELO WATUA BARCELONA

●●●Klabu hiyo imetangaza baada ya tarehe ya mwisho ya kufungwa dirisha kubwa la usajili...

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imekamilisha usajili wa mkopo wa wachezaji wa kimataifa wa Ureno, Joao Felix na Joao Cancelo, klabu hiyo imetangaza baada ya tarehe ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha kubwa la usajili ya majira ya joto, Ijumaa.

Felix amewasili kutoka Atletico Madrid na Cancelo kutoka Manchester City. Mikopo yote miwili itakuwa hadi mwisho wa msimu na haijumuishi chaguzi za kufanya uhamisho kuwa wa kudumu, Barcelona ilithibitisha.

Felix alikua mchezaji wa rekodi ya klabu ya Atletico alipojiunga kwa ada ya euro milioni 126 kutoka Benfica Julai 2019, lakini alijitahidi kufanya matokeo yaliyokusudiwa, akifunga mabao 34 katika mechi 131 za Atletico.

Alipelekwa kwa mkopo Chelsea Januari, ambapo alitolewa kwa kadi nyekundu mara ya kwanza na hakuweza kurekebisha masuala yao ya upachikaji mabao, akifunga mara nne pekee katika mechi 20.

Chelsea ilimteua Mauricio Pochettino msimu huu wa joto, na kocha huyo raia wa Argentina alisema hataki kumsajili mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Felix anawasili Barca huku kukiwa na kuondoka kwa Ousmane Dembele, aliyeondoka kwenda PSG mwezi uliopita, na Ansu Fati, aliyejiunga na Brighton kwa mkopo Ijumaa.

Kuwasili kwa Cancelo kunakomesha harakati za klabu hiyo ya LaLiga kutafuta beki wa kulia msimu huu wa joto.

Kocha wa Barca, Xavi Hernandez amekuwa na nia ya kuimarisha chaguo lake kwenye nafasi hiyo, baada ya kuwatumia mabeki wa kati Jules Kounde na Ronald Araujo kwenye nafasi hiyo, na kumruhusu Sergino Dest kujiunga na PSV Eindhoven.

Pia katika siku ya mwisho, Barcelona ilitangaza kumsajili kwa mkopo beki Mamadou Fall kutoka klabu ya MLS, LAFC. Fall mwenye umri wa miaka 20, atajiunga na timu B ya Barcelona kwa mkopo kwa msimu huu na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu ujao.

Mzaliwa huyo wa Senegal, Fall amecheza mechi 36 za Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS, baada ya kujiunga nayo 2021. Tayari ana uzoefu nchini Hispania, akiwa amecheza kwa mkopo Villarreal msimu uliopita.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
ASTON VILLA
1 | 1.75
X | 4.23
2 | 4.13

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AMRABAT MALI YA MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imekamilisha mkataba wa mkopo wa msimu mzima kwa kiungo wa Morocco, Sofyan Amrabat kutoka Fiorentina, klabu hizo zilitangaza siku ya tarehe ya mwisho ya uhamisho Ijumaa.

United italipa ada ya mkopo ya euro milioni 10 kukiwa na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu ujao kwa euro milioni 20 pamoja na nyongeza ya euro milioni 5, vyanzo viliiambia ESPN.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United walimsajili Amrabat mwenye umri wa miaka 27, baada ya kukubali kuhama kwa Dean Henderson kwenda Crystal Palace.

Henderson alijiunga na Palace siku ya Alhamisi kwa mkataba ambao unaweza kupanda hadi pauni milioni 20.

"Ni heshima kubwa kuwa mchezaji wa Manchester United," alisema Amrabat.

"Nimelazimika kuwa mvumilivu kwa wakati huu, lakini mimi ni mtu ambaye husikiliza moyo wangu kila wakati na sasa ninawakilisha klabu ya ndoto zangu.

"Mimi ni mchezaji mwenye shauku, nataka kuleta nguvu hiyo kwenye kikosi, na nitaweka kila kitu katika kila hatua nitakayoichukua kwa timu."

# Liverpool yapuuzia ofa Al Ittihad

**LIVERPOOL, England**



KLABU ya Liverpool imekataa ofa yenye thamani ya hadi pauni milioni 150 kwa ajili ya Mohamed Salah kutoka klabu ya Al Ittihad ya Saudi Arabia, vyanzo vimeiambia ESPN.

Salah mwenye umri wa miaka 31, amekuwa akihusishwa na kuhamia kwa mabingwa hao wa Saudia wiki za hivi karibuni, licha ya msisitizo wa kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp kwamba mchezaji huyo hataruhusiwa kuondoka Anfield.

Lakini wakati Liverpool walisema wanafahamu kuhusu nia ya Al Ittihad kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri, hakuna ofa rasmi iliyowasilishwa kumsajili mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea na AS Roma.

Hatimaye Al Ittihad walitoa ofa yao Ijumaa asubuhi, na kutoa kitita cha pauni milioni 100 kwa Salah na motisha ya ziada na kuifanya kuwa na thamani ya pauni milioni 150.

Lakini vyanzo vimeiambia ESPN ofa ya Salah imekataliwa na suala hilo limefungwa, na chanzo cha Liverpool kiliiambia ESPN, "Mchezaji hauzwi."

Al Ittihad walikuwa na nia ya kumuunganisha Salah na Karim Benzema, mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, ambaye alijiunga na klabu hiyo yenye maskani yake Jeddah akitokea Real Madrid kama mchezaji huru mapema msimu huu wa joto.

Salah pia angeungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Liverpool, Fabinho, ambaye aliondoka Anfield na kwenda Al Ittihad wakati wa dirisha hili la usajili, lakini Liverpool wameondoa uwezekano wowote wa dili kufutwa.

Klopp alisema mapema Ijumaa bado ana wasiwasi kuhusu tishio linaloletwa na klabu za Saudi Arabia, kutokana na dirisha lao la uhamisho kubaki wazi hadi katikati ya Septemba.

Salah, ambaye mkataba wake na Liverpool unamalizika Juni 2025, bado hajazungumza chochote kuhusu nia ya Al Ittihad.

## HABARI MICHEZO

Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# BIASHARA UNITED YAPANIA KUREJEA LIGI KUU 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Shirikisho la soka nchini kupitia bodi ya Ligi kutoa ratiba ya ligi ya 'Championship' inayotarajiwa kuanza Septemba 10, klabu ya Biashara United imeweka malengo yao ya kutaka kurejea ligi kuu msimu ujao.

Biashara United itakayoshiriki ligi ya Championship baada ya kushuka daraja misimu miwili iliyopita, itaanza kampeni yake ya kurejea ligi kuu kwa kucheza na Mbuni FC Septemba 10 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Amani Josia amesema usajili bora walioufanya msimu huu unawapa matumaini makubwa ya kuweza kufanikisha malengo hayo waliyoyakusudia.

"Napenda nitoe shukrani zangu kwa Rais wa Klabu pamoja na viongozi wote kwa sapoti kubwa waliyotupa, hasa kwenye usajili na kufanikiwa kupata wachezaji wazuri, msimu huu tutakuwa na kikosi mchanganyiko, wapo wazoefu na vijana wanaochipukia wenye njaa na mafanikio, kwa hiyo naamini mchanganyiko huo utatupa mseto mzuri wa kufanya vizuri kwenye Ligi daraja la Kwanza," alisema kocha huyo.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanarejea Ligi kuu msimu ujao na kurudisha furaha kwa mashabiki wao na wananchi wa mkoa wa Mara.

Aidha, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kujazana uwanjani wakati timu hiyo inacheza ili kuwapa hamasa wachezaji.

"Mashabiki watarajie kuwa na timu yenye muunganiko mzuri na inayopambana ikiwa na nia kurejea katika Ligi Kuu, hivyo tunawaomba wajitokeze na kujazana uwanjani kwa ajili ya hamasa kila inapocheza kwenye uwanja wetu," alisema Josia.

Biashara United huutumia Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara kama uwanja wake wa nyumbani.

Timu hiyo ilishuka daraja msimu wa 2021/22, baada ya kupanda na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza 2019/20.

Msimu mmoja tu baada ya kupanda ilishika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi na kufanikiwa kukata tiketi ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika na kufanya vyema ingawa ikashindwa gharama za kusafiri kwenda nchini Libya kucheza mchezo wa marudiano dhidi ya Al Ahli Tripoli na kuondolewa kwenye mashindano hayo licha ya kushinda mabao 2-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.



Vijana wakicheza mpira katika viwanja vya Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

## Gamondi ashtukia

INATOKA UK. 24

ajili ya kuweza kuongeza stamina katika miili ya wachezaji wangu, Safari yetu kuelekea kwenye malengo yetu ni kubwa hatuhitaji kukaa kusubiria ratiba zifikie ndiyo turudi kujipanga, tunachokiangalia ni kwa jinsi gani tunaweza kupata matokeo kwa kuhakikisha timu yetu inakuwa imara muda wote ndiyo maana ratiba zetu tunaendelea nazo, " alisema Gamondi.

Mchezo wa marudiano utakaotoa picha kamili ya nani anatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo utachezwa kati ya Septemba 25-27 Jijini Dar es Salaam .

## Manula kurejea Novemba

INATOKA UK. 24

wa Mo Arena, huku akitarajiwa kuwa anaweza kuwa fiti na kukaa langoni mwezi Novemba.

Manula alionekana jana akifanya mazoezi yake binafsi pembeni, akisimamiwa na madaktari, makocha na watu wa benchi la ufundi ambao walikuwa karibu naye.

Daktari wa klabu hiyo, Edwin Kagabo amesema mchezaji huyo yupo kwenye asilimia 80 kuelekea kwenye 90 ya kupona kabisa.

"Katika matibabu yake tupo kwenye asilimia 80 tunaelekea kwenye 90 ya kuweza kupona kabisa, atafanya mazoezi haya kwa muda wa wiki tatu au nne hivi ili mwili mzima ukiunganisha na sehemu aliyoumia vyote vikae sawa na kuimarisha misuli yote ya mwili, tutegemee mwezi mmoja na wiki moja anaweza kuungana na wenzake kwenye mazoezi," alisema daktari huyo.

Daktari huyo amesema mazoezi anayoyafanya ni awamu ya tatu ya tiba baada ya kufanyiwa upasuaji na kuanza mazoezi tiba na sasa anaendelea na mazoezi hayo lakini ya uwanjani zaidi chini ya uangalizi wa madaktari.

Manula aliumia Aprili 7 mwaka huu katika mchezo wa Kombe la FA kati ya timu yake dhidi ya Ihefu uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam ambapo hakumaliza mechi, Simba ikishinda mabao 5-1.

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 03/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 1723 | Utrecht vs Feyenoord | 4.37 | 4.17 | 1.61 |
| 14:00 | 4104 | Toulouse vs Clermont Foot | 2.01 | 3.59 | 3.64 |
| 14:30 | 1577 | Greuther Furth vs Hannover | 1.92 | 3.84 | 3.34 |
| 14:30 | 1843 | Hamburger SV vs Hansa | 1.46 | 4.62 | 5.63 |
| 15:00 | 2870 | FC Andorra vs Tenerife | 2.17 | 2.97 | 3.42 |
| 15:00 | 3831 | Silkeborg vs Hvidovre IF | 1.44 | 4.41 | 6.42 |
| 15:00 | 3890 | Girona vs Las Palmas UD | 1.67 | 3.79 | 5.33 |
| 15:00 | 4211 | Lyngby vs Nordsjalland | 4.32 | 3.56 | 1.78 |
| 15:30 | 1583 | FC Volendam vs Twente | 4.84 | 4.35 | 1.53 |
| 15:30 | 5333 | Fortuna Sittard vs Ajax | 6.35 | 4.96 | 1.37 |
| 16:00 | 1643 | Liverpool vs Aston Villa | 1.75 | 4.23 | 4.13 |
| 16:00 | 1688 | Le Havre vs Lorient | 2.72 | 3.24 | 2.67 |
| 16:00 | 2808 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 1.96 | 3.39 | 4.06 |
| 16:00 | 3752 | Lille vs Montpellier | 1.79 | 4.02 | 4.12 |
| 16:00 | 5720 | Metz vs Reims | 3.91 | 3.65 | 1.92 |
| 16:30 | 3104 | Eintracht Frankfurt vs FC Koln | 2.21 | 3.34 | 3.34 |
| 17:00 | 2559 | Brondby vs Randers | 1.69 | 3.71 | 4.71 |
| 17:00 | 5769 | Bodrumspor vs Umraniyespor | 1.97 | 3.37 | 3.27 |
| 17:15 | 3224 | Eibar vs Leganes | 1.99 | 3.07 | 3.81 |
| 17:15 | 4112 | Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.25 | 3.09 | 2.39 |
| 17:30 | 2468 | GD Chaves vs Moreirense | 2.38 | 3.19 | 2.84 |
| 17:30 | 2655 | Vilaverdense FC vs Nacional Madeira | 2.07 | 3.27 | 3.27 |
| 17:30 | 4412 | GD Estoril vs Boavista | 2.37 | 3.23 | 2.83 |
| 17:45 | 1769 | Vitesse Arnhem vs AZ Alkmaar | 3.53 | 3.58 | 1.90 |
| 18:05 | 3524 | Nice vs Strasbourg | 1.96 | 3.60 | 3.80 |
| 18:30 | 1806 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.15 | 3.30 | 2.33 |
| 18:30 | 1921 | Arsenal vs Manchester Utd | 1.86 | 3.79 | 4.04 |
| 19:00 | 5910 | Copenhagen vs Viborg FF | 1.64 | 3.92 | 4.78 |
| 19:15 | 1465 | Samsunspor vs Istanbulspor | 1.93 | 3.56 | 3.51 |
| 19:15 | 4127 | Besiktas vs Sivasspor | 1.50 | 4.18 | 5.64 |
| 19:15 | 5338 | Corum Bld vs Genclerbirligi | 1.98 | 3.32 | 3.27 |
| 19:30 | 1633 | Torino vs Genoa | 2.06 | 3.24 | 3.91 |
| 19:30 | 3674 | Inter vs Fiorentina | 1.73 | 3.79 | 4.82 |
| 19:30 | 4248 | Atletico Madrid vs Sevilla FC | 1.50 | 4.44 | 6.40 |
| 19:30 | 4401 | Spezia vs Como | 1.73 | 3.45 | 4.53 |
| 19:30 | 5411 | Ternana vs Bari | 2.63 | 3.04 | 2.63 |
| 20:00 | 5867 | Porto vs FC Arouca | 1.29 | 5.13 | 8.61 |
| 21:00 | 1738 | Midtjylland vs Aarhus | 2.39 | 3.32 | 2.81 |
| 21:45 | 2314 | Lyon vs Paris St Germain | 5.08 | 4.49 | 1.59 |
| 21:45 | 2680 | Sanliurfaspor vs Erzurum BB | 1.68 | 3.52 | 4.33 |
| 21:45 | 2733 | Empoli vs Juventus | 4.72 | 3.69 | 1.76 |
| 21:45 | 3196 | Altay vs Goeztepe | 2.97 | 3.17 | 2.18 |
| 21:45 | 4010 | Lecce vs Salernitana | 2.03 | 3.35 | 3.86 |
| 21:45 | 4236 | Hatayspor vs Adana Demirspor | 3.00 | 3.72 | 2.07 |
| 21:45 | 4888 | Cittadella vs Venezia | 2.44 | 3.07 | 2.82 |
| 21:45 | 5682 | Ankaragucu vs Fenerbahce | 4.22 | 3.91 | 1.69 |
| 22:00 | 1396 | Huesca vs Mirandes | 2.02 | 3.17 | 3.57 |
| 22:00 | 2343 | Corinthians vs Palmeiras | 3.24 | 3.09 | 2.14 |
| 22:00 | 4577 | Osasuna vs Barcelona | 4.73 | 3.84 | 1.73 |
| 22:30 | 4264 | Sporting Braga vs Sporting Lisbon | 2.93 | 3.47 | 2.19 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Septemba 3, 2023

Nipashe




## Joao Felix, Cancelo watua Barcelona

UKURASA 21




Mshambuliaji wa Al Nassr ya Saudi Arabia, Cristian Ronaldo akimtoka beki wa Al Taawoun FC Hassan Kadesh kwenye mchezo wa Ligi kuu ya nchini humo juzi usiku, timu ya Ronaldo ilifungwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# KABLA KUWAKABILI AL MERREIKH, GAMONDI ASHTUKIA KITU MAPEMA

### Awabadilishia mazoezi wachezaji wake kusaka pumzi, stamina...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha timu yake inafikia malengo kwenye michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi ni kama ameshtukia kitu kuelekea mchezo wao dhidi ya Al Merreikh na sasa amewabadilishia mazoezi wachezaji wake ambapo amewahamishia ufukweni kutafuta pumzi zaidi na stamina kabla ya mchezo huo.

Yanga inajiandaa kuumana na Al Merreikh ya Sudan kati ya Septemba 15-17 kwenye hatua ya kwanza ya michuano hiyo kuwania kutinga hatua ya makundi.

Akizungumza jana jijini Dar es salaam, Gamondi amesema anataka kuona wachezaji wake wanakuwa fiti kwenye kila idara kabla ya mchezo huo wa kwanza watakaoanzia ugenini ambao anaamini utakuwa mgumu.

"Tupo kwenye programu maalum kuhakikisha wachezaji wangu wanakuwa fiti, hatuwezi kufikia malengo yetu kama hatutakuwa timamu katika kila idara uwanjani, wapinzani wetu ni wazuri na ni timu kubwa, hii ndio sababu nimekuwa nikiwabadilishia wachezaji wangu mazoezi katika kipindi hiki cha maandalizi," alisema Gamondi.

Kocha huyo ambaye anaonekana amepania kuweka rekodi ya Yanga kutinga katika hatua ya makundi kwa mara ya kwanza kwenye michuano hiyo, alianza programu yake maalum ya mazoezi juzi Jumamosi kwa kuwapeleka wachezaji wa timu hiyo 'Gym' huku akionekana kutoa maelekezo zaidi kwa nyota wake wawili, Max Nzengeli na Pacome Zouzoua.

Gamondi, alisema hawatakuwa na muda wa kupumzika zaidi ya siku za wikiendi pekee kwa kuwa mikakati yake ni kujenga timu imara itakayoweza kushindana na kupata matokeo wakati wowote uwanjani.

Alisema anahitaji wachezaji wake kuwa na utimamu mzuri wa mwili, wanakuwa fiti na kufuata maelekezo yake wakati wakiwa uwanjani.

"Wachezaji nawapumzisha siku mbili, Jumamosi na Jumapili, Jumatatu (kesho) asubuhi tutafanya mazoezi ufukweni kwa

INAENDELEA UK 23

## Manula kurejea Novemba, Aubin Kramo aanza kutupia

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA namba moja wa klabu ya Simba, Aishi Manula anatarajiwa kurejea uwanjani kwenye michezo ya ushindani Novemba, lakini habari njema kwa mashabiki wa timu hiyo ni kurejea kwa kasi kwa winga wake Aubin Kramo.

Kramo raia wa Ivory Coast aliyesajiliwa msimu huu akitokea Asec Mimosas alikuwa hajacheza mechi yoyote baada ya kuumia mazoezini, lakini jana asubuhi kwenye mchezo wa kirafiki alifunga bao katika mechi ya kirafiki dhidi ya Kipanga ya Zanzibar kwenye uwanja wa Mo Arena, Dar es Salaam.

Tangu atue Simba alikuwa ameichezea timu hiyo kwa dakika 10 tu, akiingia kwenye mechi dhidi ya Power Dynamos kuchukua nafasi ya Kibu Denis dakika ya 80, baada ya hapo hakuonekana tena katika michuano ya Ngao ya Jamii na mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar na Dodoma Jiji.

Katika mechi ya jana, Simba ilishinda mabao 3-0, Kramo akitupia dakika ya 70 kwa mpira wa faulo likiwa ni bao la tatu kwenye mechi hiyo.

Moses Phiri ambaye naye ameanza taratibu kurejea kwenye kikosi baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu kwa majeraha, alitupia bao la kwanza dakika ya 21, huku Luis Miquissone ambaye pamoja na kucheza mechi kadhaa bila kufunga, alianza kufungua akaunti yao ya mabao kwa kupachika bao dakika ya 41.

Mechi hiyo imetokana na programu ya mwalimu Roberto Oliveira ambaye alitaka kikosi chake kupata mechi mbili au tatu za kirafiki kwa ajili ya kuwaweka sawa kwa utimamu wa mwili na pumzi wachezaji wake ambao wamekaa muda mrefu bila kucheza.

Zipo taarifa kuwa huenda Simba ikacheza mechi nyingine dhidi ya Gor Mahia ya Kenya.

Wakati huo huo, golikipa namba moja wa timu hiyo, Manula ameanza mazoezi kwenye Uwanja

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >